SportPesa
TZS. 619,207,580
BET LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Kesi** madai ya mauaji mama mzazi yaanza kunguruma

UKURASA 3



**Wanne watajwa kumrithi Solskjaer**

UKURASA 23


# Nipashe

Jumatano Oktoba 27, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580746

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




## KESI YA MBOWE

# Mawakili utetezi waibua hoja saba

• **ACP** Kingai adai Mbowe alitaka kumdhuru Sabaya kwa poda yenye sumu... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**UJERUMANI YAIMWAGIA TANZANIA BIL. 190/-**

UJERUMANI imeipatia Tanzania msaada wa Euro milioni 71, sawa na Sh. bilioni 190.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi...

UKURASA WA 7

**SABAYA KIZIMBANI TENA KESI UHUJUMU**

KESI ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole...

## Maelfu wapata mikopo elimu ya juu awamu III

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, alipomtembelea kumjulia hali nyumbani kwake Oysterbay, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni mke wake, Regina Lowassa. **PICHA: IKULU**

# Mbivu mbichi waliovujisha mitihani utabibu Jumatatu

UKURASA 2

**MICHEZO** **GOMES AFUNGUKA MAZITO KUTIMULIWA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe (katikati), akiwa chini ya ulinzi wa askari, baada ya kuwasili katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, Sinza mkoani Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi inayomkabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mawakili utetezi waibua hoja saba

**Na Kulwa Mzee**

KAMISHNA Msaidizi wa Polisi (ACP) Ramadhan Kingai, amedai Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, alitoa maelekezo ya kumdhuru aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, kwa kumpulizia poda ya sumu usoni.

Amedai kuwa kiongozi huyo wa CHADEMA alitoa maelekezo hayo kwa madai Sabaya ni kikwazo kwake kulipata Jimbo la Hai.

Hata hivyo, kutokana na madai hayo, upande wa utetezi umeibua hoja saba ulizozielekeza kwa shahidi huyo, ukitaka ufafanuzi.

Kingai alidai hayo jana alipotoa ushahidi Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga kwa kuongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando.

Alidai katika maelezo ya onyo aliyotoa mshtakiwa wa pili, Adamu Kasekwa, maarufu Adamo, Julai 24, 2020, akiwa na mshtakiwa wa tatu, Mohammed Ling'wenya, walikutana na Luteni Dennis Urio Morogoro, na aliwafahamisha kuna kazi ya ulinzi wa kiongozi kwa Mbowe.

Shahidi huyo anadai Urio aliwapa Sh. 87,000 kila mmoja kwa ajili ya kwenda Moshi na walifika Moshi saa 10 alfajiri wakapokewa na dereva wa Mbowe aliyeitwa Willy akiwa na Pickup ya Chadema M4C, wakapelekwa Hoteli ya Aishi kulala.

Katika maelezo hayo, Kasekwa alidai asubuhi walitambulishwa kwa Mbowe na mshtakiwa Halfani Bwire na ilipofika saa tano usiku, walifanya kikao wakiwa watu watano.

"Tulifanya kikao na Mbowe Julai 24, mwaka 2020, tukiwa watano, Mbowe, Ling'wenya, Moses Lijenje na Bwire, alitupa maelekezo. Alisema Sabaya anamvuruga sana, anawavuruga wapigakura wake wa Jimbo la Hai, amesababisha fedha za ruzuku za CHADEMA zimeshushwa.

"Anayofanya Sabaya yanamtia wasiwasi, yanahatarisha kuukosa ubunge, tuweke miundombinu ya kumdhuru ili asifanikiwe kufanya mambo yake ili Mbowe apite.

"Alituelekeza kumdhuru kwa namna yoyote ile, tulipanga kumdhuru kwa kumpulizia poda ya sumu usoni. Julai 26, 2020, tulirudi Dar es Salaam.

"Tulipofika tulipewa Sh. 200,000 kwa ajili ya maandalizi ya mavazi ya kumpokea Tundu Lissu Uwanja wa Ndege. Julai 31, 2020 tulirudi Moshi na tulipewa nauli Sh. 78,000.

"Tulipofika Moshi tulimkuta Mbowe na Bwire wako Aishi Hoteli. Alfajiri ya Agosti Mosi, 2020, Mbowe wakati anataka kurudi Dar es Salaam, alituita alituelekeza azma yake ya kumdhuru Sabaya, alituonyesha picha ya Sabaya kupitia simu yake ya kiganjani, alituambia anapatikana katika Klabu ya Kokoliko.

"Mbowe alituacha Moshi, tulianza kumtafuta Sabaya Boma Ng'ombe, Kokoliko na Way Stone hatukumwona, kazi hiyo tulifanya Agosti 3 na 4 mwaka 2020 na Agosti 5 tuliamua kwenda Rau Madukani kwa dada yake Ling'wenya ili kubana matumizi kwa sababu tuliachiwa kiasi kidogo, Sh. 150,000 isingetosha kujikimu.

"Alituambia baada ya kumaliza kazi hiyo atatupa kazi nyingine ya kulipua vituo vya mafuta, kukata miti barabarani, kuratibu maandamano yasiyo na kikomo ili kuonyesha serikali imefeli kuelekea Uchaguzi Mkuu," alidai hayo yalikuwa maelezo ya Kasekwa.

ACP Kingai alidai kuwa Kasekwa alikiri kukamatwa na polisi Agosti 5, 2020 wakiwa Rau Madukani, alikiri kukutwa na pisto yenye risasi tatu, alikiri kukutwa na dawa za kulevya aina ya heroine kete 58.

Anadai walimtafuta mshtakiwa Bwire na kufanikiwa kumkamata, walipofanya upekuzi nyumbani kwake maeneo ya Temeke, walimkuta akiwa na sare za JWTZ pamoja na vifaa vingine vya jeshi na vitendo vya kigaidi walipanga kufanya Moshi, Dar es Salaam, Mbeya na Mwanza.

**HOJA SABA ZA UTETEZI**

Hata hivyo, upande wa utetezi uliibua hoja saba wakati ukimhoji shahidi hiyo, ikiwa ni pamoja na washtakiwa kukamatwa wakiwa hawana vifaa vyovyote vya ulipuaji, ukataji miti na kuchukuliwa alama za vidole ili kujiridhisha kama walishika silaha husika.

Akihojiwa na Wakili wa Utetezi, Jeremiah Mtobesya, ACP Kingai alidai ushiriki wa Luteni Dennis Urio ulikuwa ni kuwatafuta vijana wa kufanya kazi kwa Mbowe na kuwapa fedha zilizotoka kwa Mbowe.

Akihojiwa na Wakili John Mallya, ACP Kingai alidai alichukua maelezo ya onyo kupitia Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 57 na 58 sura ya 20 ya mwaka 2018, lakini imekosewa na wachapaji ilipaswa kuwa mwaka 2002 na si 2018.

Akihojiwa na Wakili Peter Kibatala, ACP Kingai alidai hawajawakamata washtakiwa wakiwa na kifaa chochote cha ulipuaji wa vituo vya mafuta, kukata miti wala kipeperushi cha kufanya maandamano mikoa ya Dar es Salaam, Moshi, Arusha, Morogoro na Mwanza.

Alidai katika ushahidi wake hakuzungumzia lolote kuhusu washtakiwa wote kukutana Arusha na hafahamu kama washtakiwa waliwahi kufanya kikao Morogoro.

ACP Kingai alidai alitoa onyo kwa kosa la kufanya ugaidi, lakini hakumwonya Kasekwa kwa kufanya kikao na hakumwonya kwa shtaka la nne la kukutwa na pisto na aliongeza kuwa hajawahi kuchukua alama za vidole kujiridhisha kwamba Kasekwa aliishika silaha hiyo.

Pia shahidi huyo wa kwanza alidai walichukua simu za watoto wa Mbowe na baada ya uchunguzi, walibaini hazihusiani na kesi hiyo lakini simu hizo hazijarudishwa na alipokea maombi ya kuzitaka wiki mbili au tatu zilizopita.

Alidai hakuwahi kumfahamisha Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kesi hiyo na upelelezi wake wala hakuwahi kutoa taarifa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama kuhusu tukio la kumdhuru Sabaya.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Bwire, Kasekwa, Ling'wenya na Mbowe ambao wanakabiliwa na mashtaka sita yakiwamo ya kula njama kufanya vitendo vya kigaidi, ikiwamo kulipua vituo vya mafuta na kumdhuru Sabaya. Kesi hiyo inatarajiwa kuendelea leo.

## Mbivu mbichi waliovujisha mitihani utabibu Jumatatu

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, imesema Jumatatu ijayo itaweka wazi watu wote waliohusika na uvujaji wa mitihani ya utabibu nchini.

Waziri mwenye dhamana, Dk. Dorothy Gwajima, alisema hayo mjini hapa wakati akizindua kituo cha afya cha elimu Masafa, kilichoko Mkundi, Manispaa ya Morogoro.

Alisema hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa wote watakaobainika kuhusika na uvujaji huo wa mitihani na kubainisha kuwa wizara imeshaunda kamati itakayoandaa ripoti na kuikabidhi kwake na anatarajia kuisoma kwa wananchi.

Dk. Gwajima alisema vyuo vya kada ya afya vinatarajiwa kutoa watumishi watakaokuja kuwahudumia Watanzania na kitendo cha kuwapatia watu majibu ya mitihani bila kufanya na kufaulu mitihani hiyo ni kosa kubwa sana.

Kuhusu kituo cha elimu Masafa alichozindua ambacho pamoja na samani zilizomo, kimegharimu kiasi cha Dola za Kimarekani milioni tatu.

Aliwaagiza viongozi wake kuboresha mifumo ili waweze kuzalisha watumishi bora zaidi na kuwaendeleza zaidi waliopo kazini.

Awali Mkurugenzi wa Mafunzo kutoka wizara hiyo, Dk. Sastore Laizer, alisema kituo hicho kitasaidia wanafunzi na watumishi wa kada ya afya kuongeza elimu na kutoa watumishi bora.

"Tunaomba zaidi wizara isaidie kutatua changamoto kadhaa zinazokikabili kituo hiki hasa Bweni, huduma ya majisafi na salama, barabara na usafiri," alisema Dk. Laizer.

Mkuu wa kituo hicho, Ndementria Verman, alisema uwapo wa kituo hicho umewezesha watumishi wa kada ya afya walioshindwa kujiendeleza kutokana na sababu mbalimbali kufanya hivyo sasa wakiwa wanaendelea na kazi.

## HABARI KITAIFA

# Kesi mauaji mama mzazi yaanza kunguruma kortini

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imeanza kusikiliza kesi ya mauaji inayomkabili, Manoni Isheli, anayeshtakiwa kwa madai ya kumuua kwa makusudi mama yake mzazi, Njombile Manoni (90) kwa kumcharanga mapanga kichwani na kufariki dunia papo hapo.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani jana mbele ya Jaji wa Mahakama hiyo, Fredrick Manyanda, hata hivyo alikana kosa hilo na kupelekwa mahabusu kutokana na kesi yake kutokuwa na dhamana.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali James Pallangyo, ulidai una mashahidi wawili pamoja na vielelezo vitatu. Upande wa utetezi wa mshtakiwa ukiongozwa na wakili wa kujitegemea, Penina Mashimba, ulidai uko tayari kusikiliza mashahidi wawili wa upande wa Jamhuri.

Jaji Manyanda alikubaliana na ombi hilo na kuanza kusikiliza mashahidi wawili wa upande wa Jamhuri.

Shahidi wa kwanza upande wa Jamhuri Sajenti Saidi akiongozwa na Wakili wa Serikali Pallangyo, alidai Oktoba 14, 2015 majira ya mchana alipata taarifa kuwa kuna mauaji yametokea katika Kijiji cha Ngura, Wilaya ya Geita na akiwa na askari saba wakiongozwa na Mkuu wa Upelelezi wa wilaya hiyo, walipofika kijijini hapo walimkuta mama mmoja Njembele Kanoni (90) amefariki dunia akiwa na majeraha kichwani.

Saidi alidai alipewa maagizo na Mkuu wa Upelelezi wa wilaya hiyo amwandikie maelezo mume wa marehemu Isheli Barabara (96) na kudai siku ya tukio alikuwa anaoga na kusikia sauti ya mke wake Kanoni (ambaye sasa ni marehemu) akiomba msaada.

Alidai alipotoka nje alimuona mtoto wake, Manoni Isheli akitoka ndani huku akikimbia na alipomuita hakusimama, ndipo akaingia ndani na kukuta mke wake amekatwa mapanga kichwani damu zikivuja.

Alisema alitoka nje na kupiga yowe na wananchi walifika na kukuta mama huyo ameshafariki dunia.

Aidha, walitoa taarifa polisi ambao waliuchukua mwili wa marehemu na kuupeleka Hospitali ya Mkoa wa Geita kwa uchunguzi.

Alidai kuwa Oktoba 18, 2015 akiwa katika kituo cha polisi Geita majira ya saa nane mchana aliletwa mshtakiwa Kanoni Isheli akikabiliwa na kosa la mauaji ya mama yake mzazi.

Pia, alidai ilipofika majira ya saa tisa mchana alipewa maagizo na Mkuu wa Upelelezi ili aandike maelezo ya mtuhumiwa huyo na kwamba mshtakiwa alikiri kumuua mama yake mzazi kwa madai alikuwa akiwaroga watoto wake.

Alidai mshtakiwa huyo baada ya kuona watoto wake wanaumwa kila wakati aliamua kwenda kwa mganga wa kienyeji na kuambiwa mama yake mzazi ndiye anawaroga watoto wake.

Aliendelea kudai kuwa mshtakiwa huyo baada ya kupata taarifa hizo alichukua panga na kwenda hadi nyumbani kwao na kumkuta mama yake mzazi akiwa ndani ya nyumba ndipo alipomkatakata kichwani na kufariki dunia papo hapo na kutokomea kusikojulikana.

Hata hivyo, alidai baada ya muda ndugu zake walifanya msako na kufanikiwa kumkamata na kumpeleka kituo cha polisi.

Shahidi wa pili wa upande wa Jamhuri, Daktari wa Hospitali ya Mkoa wa Geita, Christopher Matola akiongozwa na Wakili wa Serikali Pallangyo, alidai Oktoba 15, 2015 majira ya saa tano asubuhi alikuwa hospitalini na kupewa maagizo na Mganga Mkuu wa hospitali hiyo akachunguze mwili wa marehemu.

Matola alidai kuwa alienda chumba cha kuhifadhia maiti pamoja na ndugu wa marehemu wawili, askari polisi wawili, wahudumu wawili pamoja yeye.

Baada ya uchunguzi alibaini kuwa Matola alifariki dunia kwa kuvuja damu nyingi kutokana na jeraha kubwa lililokuwa nyuma ya kichwa, ambalo lilitokana na kukatwa na panga au kitu chenye ncha kali.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi leo kwa ajili ya kuendelea na shahidi wa kwanza upande wa Jamhuri.

## KUMBUKUMBU






**Wilneza Mathew Mrema Baba yetu mpendwa**, ni miaka mitano (5) umefikisha sasa tangu ulipotutoka tarehe 26/10/2016 Mwenyezi Mungu alipotwaa roho yako nzuri na kukupa pumziko la milele; hakuna mtu ajuae ni kiasi gani tunaumia mioyoyoni mwetu; hakuna anayejua maumivu ambayo tumejeruhiwa tangu kutwaliwa kwako baba yetu mpenzi; maisha hayajawahi kuwa sawa miyoyoni mwetu kumbukumbu yako inatukumbusha mema yako mazuri kwetu, upendo wa agape na mengi uliotuachia baba; Hakuna siku mpendwa Baba ipitayo bila kufikiria juu yako. Unakumbukwa sana na mke wako mpenzi Eva, watoto wako Lucy, Goodie, Irene, Denis, Monica, Sia, David, Walter, wajukuu wako, Kaka na dada yako kipenzi Edna, ndugu, jamaa na marafiki pamoja na uongozi na wafanyakazi wa Network Freight Forwarders Ltd.

# Maelfu wapangiwa mikopo elimu ya juu awamu III

**Na Mary Geofrey**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imetangaza orodha ya awamu ya tatu ya wanafunzi 15,261 wa mwaka wa kwanza, waliopangiwa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 37.9 kwa mwaka wa masomo 2021/22.

Mkurugenzi wa Upangaji na Utoaji Mikopo HESLB, Dk. Veronica Nyahende, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, alibainisha kuwa orodha hiyo imefanya jumla ya wanafunzi wapya wa mwaka wa kwanza waliopangiwa mikopo kufikia 60,356, yenye thamani ya Sh. bilioni 157.3.

Dk. Nyahende aliongeza kuwa HESLB tayari imeanza kupeleka fedha za wanafunzi waliopangiwa mikopo kwa awamu zote tatu katika vyuo mbalimbali nchini.

Aliwataka wanafunzi kupata taarifa za kina katika akaunti walizotumia kuomba mkopo maarufu kama SIPA (Student's Individual Permanent Account), ili kujiandaa kwenda vyuoni, kwa ajili ya kujisajili.

"Orodha hii ya tatu inajumuisha wanafunzi wenye sifa zikiwamo kuwa wahitaji, wameomba kwa usahihi na wamekamilisha taratibu za udahili wa chuo kimoja," alisema.

Dk. Nyahende alisema HESLB imeshapokea fedha na kukamilisha taratibu zote, kwa ajili ya malipo ya wanafunzi na fedha za awamu zote tatu zimeanza kutumwa vyuoni.

"Serikali imeshatupatia fedha na tumeanza kuzipeleka vyuoni, lengo letu ni kuhakikisha wanafunzi wanaopangiwa wanazikuta fedha vyuoni, ambako watajisajili na kupokea fedha, ili watimize ndoto zao," alisema.

Alisema katika siku chache zijazo, wanatarajia kutangaza awamu ya nne ya wanufaika wa mikopo hiyo.

"Orodha itatolewa siku chache zijazo baada ya kukamilisha uchambuzi wa maombi unaoendelea, hivyo waombaji mikopo watembelee akaunti zao za SIPA, ili kupata taarifa kuhusu maombi yao," alisema.

Dk. Nyahende alikumbusha kuwa serikali imetenga Sh. bilioni 570, kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi 160,000.

Alisema kati yao, wanafunzi 70,000 ni wanufaika wa mwaka wa kwanza na wanafunzi zaidi ya 90,000 ni wale wanaoendelea na masomo baada ya kufaulu mitihani yao ya mwaka.

Hadi kufikia Septemba 30 mwaka huu, HESLB ilikuwa imepokea maombi mapya 88,688. Kati ya waombaji hao, 85,706 walikuwa wamejaza kikamilifu na 2,982 walitakiwa kufanya marekebisho.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA BODI YA USHAURI YA TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI TANZANIA (TAFIRI)**

Kufuatia uteuzi wa Bw. Yahaya Ibrahim Mgawe kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa Mamlaka aliyonayo chini ya Kifungu Na. 8 (3), Jedwali la Pili 1(1) (b) la Sheria ya The Tanzania Fisheries Research Institute Act No. 11 of 2016 amewateua wafuatao kuwa Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI).

1. Dkt. Hamisi Lucian Nikuli;
2. Bi. Justina Tumaini Mashimba;
3. Pro. Marcellina Mvula Chijoriga;
4. Dkt. Mectridis Fratern Mdaku;
5. Dkt. Bugwesa Zablon Katale;
6. Dkt. Lucas Albani Katera;
7. Bi. Vivian Kazi Matenge, na
8. Bw. Winfred Venant Haule.

Uteuzi huu ni wa miaka mitatu kuanzia tarehe 26 Oktoba, 2021 hadi tarehe 25 Oktoba 2024. Katibu Mkuu na Menejimenti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Sekta ya Uvuvi inawapongeza Mwenyekiti na Wajumbe kwa Uteuzi huu.

**Dkt. Rashid Tamatamah**
**KATIBU MKUU –UVUVI**

# Tanzania Commercial Bank

Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### TANZANIA COMMERCIAL BANK

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | | Robo Mwaka /Mwaka wa sasa 30/09/2021 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30/06/2021 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 41,873 | 42,425 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 64,413 | 67,804 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 112,814 | 115,988 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 78,327 | 88,611 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 435 | (35) |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 85,297 | 133,356 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 681,988 | 658,761 |
| | 12 | Mali Nyingine | 46,632 | 46,141 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 22,522 | 23,332 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,134,301** | **1,176,384** |
| B | | **DHIMA** | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| | 18 | Amana za Wateja | 755,420 | 754,781 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | 20 | Amana Maalumu | 156,088 | 212,906 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 1,300 | 5,730 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2 | 2 |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 21,005 | 20,996 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,456 | 2,254 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 26,208 | 28,567 |
| | 28 | Madeni | 60,724 | 40,920 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,023,203** | **1,066,155** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **111,097** | **110,229** |
| C. | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 28,072 | 28,072 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | - | 0 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 66,533 | 66,533 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 8,402 | 7,534 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 8,090 | 8,090 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **111,097** | **110,229** |
| | 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 171,250 | 224,141 |
| | 39 | Mikopo Chechefu | 94,680 | 82,434 |
| | 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 24,238 | 21,900 |
| | 41 | Mali Nyingine Chechefu | 83 | 27 |
| D. | | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.79% | 9.37% |
| | (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13.27% | 12.00% |
| | (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 94.46% | 91.00% |
| | (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 60.12% | 56.00% |
| | (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 79.86% | 73.29% |
| | (vi) | Ongezeko la Amana | 0.08% | 12.98% |
| | (vii) | Ongezeko la Mali | -3.58% | 15.64% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA, 2021

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-21 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 3,057 | 7,520 | 15,093 | 18,462 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 5,895 | 4,151 | 17,496 | 16,241 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (23,227) | (4,037) | (64,175) | (206,905) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (56,179) | 200,207 | 119,591 | 265,134 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (8,357) | (21,004) | (9,313) | 76,313 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (490) | (29,896) | (4,812) | (30,757) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (2,189) | (2,552) | (6,690) | (5,249) |
| | - Mengineyo (bainisha) | 46,995 | (29,015) | (95,484) | (77,032) |
| | ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(34,495)** | **125,374** | **(28,294)** | **56,208** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1,361) | (1,872) | (4,824) | (2,568) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(1,361)** | **(1,872)** | **(4,824)** | **(2,568)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (2,694) | (1,226) | (5,432) | (4,553) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | ***(2,694)*** | ***(1,226)*** | ***(5,432)*** | ***(4,553)*** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (38,550) | 122,276 | (38,550) | 49,087 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **173,727** | **51,451** | **173,727** | **23,959** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 135,177 | 173,727 | 135,177 | 73,046 |

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-21 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-21 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-20 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 33,720 | 35,163 | 99,075 | 89,420 |
| 2 Gharama za Riba | (9,762) | (11,474) | (29,008) | (27,495) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **23,957** | **23,689** | **70,067** | **61,925** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (72) | (37) | (157) | (359) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3,398) | (793) | (10,339) | (5,328) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **6,559** | **6,486** | **25,071** | **20,896** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,338 | 1,799 | 3,925 | 3,741 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,615 | 4,012 | 13,329 | 10,660 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 606 | 674 | 7,817 | 6,495 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(23,989)** | **(22,827)** | **(69,549)** | **(58,673)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 11,958 | 11,048 | 34,417 | 28,479 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 933 | 1,264 | 3,355 | 3,744 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 11,098 | 10,516 | 31,778 | 26,449 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,057** | **6,518** | **15,093** | **18,462** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 2,189 | 1,700 | 6,690 | 5,249 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **869** | **4,818** | **8,402** | **13,214** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **869** | **4,818** | **8,402** | **13,214** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1,103 | 1,049 | 1,103 | 1,049 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 31 | 172 | 299 | 471 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 47 | 44 | 47 | 44 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.08% | 0.45% | 0.77% | 1.57% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.77% | 3.88% | 7.71% | 11.79% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 59.56% | 54.81% | 56.02% | 53.19% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.64% | 2.80% | 8.12% | 9.02% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | - | - | - | | - |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | 8,402 | **8,402** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | (1,604) | **(1,604)** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **66,533** | **(0)** | **0** | **16,492** | **111,097** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **60,601** | **(0)** | **0** | **10,220** | **98,893** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 5,866 | - | - | - | **5,866** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 66 | - | - | - | **66** |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo | | | | | | (526) | **(526)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA, 2021**

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI** (Ofisa Mtendaji Mkuu) | Imesainiwa | **18.10.2021** |
| **REGINA E. SEMAKAFU** (Mkuu wa Fedha) | Imesainiwa | **18.10.2021** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE** (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | Imesainiwa | **18.10.2021** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA** Mwenyekiti wa Bodi | Imesainiwa | **18.10.2021** |
| **MS. ANNE C. MBUGHUNI** Mjumbe wa Bodi | Imesainiwa | **18.10.2021** |

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

# TANGAZO

## Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

# TARIFF GUIDE 2021

| BANK CHARGES | | |
|---|---|---|
| ITEM | FEE DESCRIPTION | TZS |
| **Minimum Opening Balance** | Quick Account | 20,000 |
| | Salary Account | FREE |
| | Tabasamu Individual | 10,000 |
| | Tabasamu Group Account | 50,000 |
| | Platinum Account | 15,000 |
| | Minor Account | 20,000 |
| | Group Account | FREE |
| | Scout Minor Account | 10,000 |
| | Scout Account | 30,000 |
| | Yanga VIP Account | 1,200,000 |
| | Yanga Members Account | 25,000 |
| | Wavuvi Account | 10,000 |
| | Current / Call Account | 100,000 |
| | Fixed Deposit Account | 100,000 |
| | WADU Account | 20,000 |

| PRODUCT NAME | MINIMUM OPENING BALANCE | MINIMUM BALANCE | MONTHLY MAINTANCE FEES |
|---|---|---|---|
| Business current account TZS | 100,000/= | 100,000/= | 200,000/= |
| Business current account USD | 100 USD | 100 USD | 20 USD |
| Personal current account TZS | 100,000/= | 50,000/= | 7,000/= |
| Personal current account USD | 100 USD | 100 USD | 5 USD |

| MAINTENANCE FEE | FEE DESCRIPTION | TZS |
|---|---|---|
| Personal Call Account | Per Month | 6,500 |
| Corporate Call Account | Per Month | 10,000 |
| **Savings Accounts** | | |
| Quick Account | Per Month | 1,560 |
| Salary Account | Per Month | 1,560 |
| Tabasamu Individual / Group Account | Per Month | FREE |
| Platinum Account | Per Month | 1,560 |
| WADU Account | Per Month | FREE |
| Minor Account | Per Month | FREE |
| Group Account | Per Month | FREE |
| Scout Junior Account | Per Month | FREE |
| Scout Senior Account | Per Month | FREE |
| Yanga VIP/ Members Account | | 1,560 |
| Yanga Members Account | | 1,560 |
| Wavuvi Account | | 1,560 |
| **Cash Deposit** | | |
| Over the Counter | Per Transaction | FREE |
| Popote Agents | Per Transaction | FREE |
| **Bank Statement** | Per Page | 2,000 |

| ATM Issuance & Replacement | | |
|---|---|---|
| Popote Card | Per Card | 5,000 |
| Yanga Card | Per Card | 20,000 |
| **Balance Enquiry** | | |
| Over the Counter | Per Enquiry | 300 |
| At the ATMs | Per Enquiry | 300 |
| At POS Branches | Per Enquiry | 150 |
| At Popote Agents | Per Enquiry | 100 |
| At TCB Popote Mobile Banking | Per Enquiry | 300 |
| Internet Banking | Per Enquiry | FREE |

| TRANSACTION | DESCRIPTION | TZS |
|---|---|---|
| **Dormant Accounts** | | |
| Activations | Per Activation | FREE |
| Dormant Account Fees | 1 year to 5 years | 1,300 |
| | 6 year to 10 years | 5,000 |
| | 11 year to 15 years | 10,000 |
| **Closing of Account** | | |
| All Accounts | Per Account | 13,000 or Equiv. in Foreign Currency |
| **Funds Transfer** | | |
| Within TCB Over the counter | Per Transaction | FREE |
| TCB Popote Mobile Banking/ Internet Banking | 500 - 10,000 | 850 |
| | 10,000.01 - 50,00 | 1,200 |
| | 50,000.01 - 100,00 | 1,500 |
| | 100,000.01 - 250,000 | 2,800 |
| | 250,000.01 - 500,000 | 4,600 |
| | 500,000.01 - 750,00 | 7,500 |
| | 750,000.01 - 1,000,000 | 10,000 |
| | | |
| From MNOs to Bank (Deposit) | | FREE |

| ATM CASH WITHDRAW | | |
|---|---|---|
| ITEM | DESCRIPTION | TZS |
| TCB ATMs | Per Transaction | 1,300 |
| Other Banks Umoja Switch ATMs | Per Transaction | 1,300 |

| OTHER ATM & NORMAL CARDS FEE | |
|---|---|
| TRANSACTION / ITEM | TZS |
| PIN Re - Issue | FREE |
| Collection of ATM Card at Non Domicile Branch | 6,500 |
| Uncollected and destroyed ATM Card | 6,500 |
| First ID Card ( Local and Foreign Currency ) | 4,000 |
| Replacement of ID Card | 2,600 |

| TRANSACTION / ITEM | TZS |
|---|---|
| Goverment Securities Transaction Handling fees | 50,000/= |

| TRANSACTION | DESCRIPTION | TZS |
|---|---|---|
| Internet Banking Registration | Per Registration | FREE |
| TCB Popote Mobile Banking Registration | Per Transaction | FREE |
| | **FEES** | |
| **TRANSACTION** | **DESCRIPTION** | **TZS** |
| Transfers | TISS - Outward | 10,000 TZS |
| | EFT - Outward | 2,000 TZS |
| | EFT - In House | 1,500 TZS |
| Standing Order | Within the Bank | FREE |
| | To other Banks | 13,000 TZS |
| Other Transfers | Internal Transfer | FREE |
| Others | Salary Handling - Cheque list | 1,000 TZS |
| | Introduction letter to Embassy, etc | FREE |

| USD TRANSACTION FEES | | |
|---|---|---|
| TYPE OF CHARGE | TRANSACTION / ITEM | CHARGES IN USD |
| **Maintenance Fee** | Savings Account | 1 |
| | Call Account | 5 |
| **Deposit Fee** | Non Account Holder | FREE |
| **Opening Balance** | | 50 |
| **Bank Statement** | | FREE |
| **Bank Statement** | Balance Enquiry - Banking Hall | FREE |
| | Confirmation letter | FREE |
| **Withdraw fees** | Below 50 | 1 |
| | 51 - 1,000 | 2.5 |
| | 1,000 - 2,250 | 5 |
| | 2,251 - 5,000 | 15 |
| | Above 5,000 | 0.25 Percent |
| **Dormant** | Dormant Account Fee | 5 |
| | Re - Activation | FREE |
| **TISS** | | 10 |

| CASH WITHDRAWAL OVER THE COUNTER | | |
|---|---|---|
| ITEM | DESCRIPTION | TZS |
| **All Accounts** | Teller Withdraw up to 10,000,000 | 2,600 |
| | Teller Withdraw form 10,000,000 - 50,000,000 | 5,000 |
| | Teller Withdraw form 50,000,001 - 100,000,000 | 15,000 |
| | TellerWithdraw above 100,000,001 | 30,000 |

| LETTER OF CREDIT ISSUED (IMPORT LCS) | CURRENT CHARGES |
|---|---|
| Charges on Draft LC | USD 60 |
| LC commission per quarter | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv. |
| LC commission per quarter with cash cover | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv. |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1% per quarter Min USD 150 or foreign eqv. |
| Other amendments | USD equiv 60 or foreign eqv. |
| Discrepancy fee per pack | USD equiv 60 or foreign eqv. |
| Document examination Fee per pack | 0 |
| Cancellation charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Non - Payment of Bills Due Date | 0 |
| Expire unutlised Letters of Credit | 0 |
| **LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS)** | **CURRENT CHARGES** |
| Advising Fee or commission | USD.200 or foreign eqv. |
| Bank clients for LC available with us | USD 150 or foreign eqv. |
| Clients for LC available with other banks | — |
| Non Bank customer | USD 250 or foreign eqv. |
| Confirmation Fee (per quarter) USD eqv. | 1% per quarter and part thereof, Min USD 250 or foreign eqv. |
| Amendment advising Fee | USD 120 or foreign eqv. |
| Cancellation Fee | USD 60 or foreign eqv. |
| Transfer Fee (per quarter) | 0.75% per quarter. Min USD 250 or foreign eqv |
| Courier services | Actual costs plus USD 10 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv |
| Document handling commission | — |
| Discrepancy Fee per document | — |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CURRENT CHARGES |
|---|---|
| Commission on LC discounting/ Negotiation | 0.75% Min USD 200 Max USD 600 or foreign eqv. |
| Negotiating Bills under an Export Letter of Credit (Discounting Bills) | — |
| **Extension - Commissions for unconfirmed LC** | 0.5% per quarter and part thereof, Min. of USD.200 or foreign eqv. |
| Extension - Commissions for Confirmed LC | 1% per quarter and part thereof Min. of USD.100 or foreign eqv. |
| **COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT)** | **CURRENT CHARGES** |
| Documents processing | 1%. Min USD 15 Max 200 |
| Courier services | Actual cost plus USD 10. |
| **Outward Documentary bills for collections (OFBC)** | |
| Document handling commission | 0.5% Min Usd 150 Max Usd 350 or foreign eqv. |
| Courier services | Actual cost plus Usd 10 or foreign eqv. |
| Chaser/ Tracer | USD 60 or foreign eqv. |
| **inward Documentary bills for collections (IFBC)** | |
| Bill Discounted Handling Commission | 0.5% Min Usd 150 Max USD 600 or foreign eqv. |
| Documents returned unpaid or unaccepted | 0 |
| For each amendment of previous instructions | 0 |
| Every presentation or reminder protest fee | 0 |
| Delivery of documents for non - customers | USD 250 or foreign eqv. |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Payment commission for documents value greater than USD 50,000 | 0 |
| Payment commission for documents value less than USD 50,000 | 0 |
| Avalisation commission per quarter or part thereof | 1,20% |
| Risk margin on acceptance (per quarter) | 1,20% |

| BANK CHARGES | | |
|---|---|---|
| TRANSACTION | DETAILS | TZS |
| Cheque Book | Per Leaf | 500 Per leaf or equivalent in foreign currency |
| Cheque Clearing Fee | Per Cheque | FREE |
| Unpaid Cheques / Insufficient Funds | Per Cheque | 150,000 TZS And Equivalent in Foreign Currency |
| Stop Payment Order | Per Cheque | 30,000 TZS per leaf Max. 300,000/= and Equivalent in Foreign currency. |

| GUARANTEE GUARANTEE ADVISING FEE (FROM OTHER BANKS) | CURRENT CHARGES |
|---|---|
| Issuance or Confirmation of Foreign Currency guarantee commission (per quarter) | 1% per quarter or part thereof Min TZS. 250,000 or USD.110 foreign eqv. |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Bid bond | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 150,000 or USD.64 foreign eqv. |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Performance, AdvancePayment and any other bank guarantees | 1.0% per quarter or part thereo Min TZS 350,000 or USD.150 foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increaseds | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD.110 foreign eqv. |
| Text amendment fee | TZS150000 or USD.64 or foreign eqvqv. |
| Other amendments | USD 60 or foreign eqv. |
| Guarantee advising fee (from other banks) | USD eqv. 200 or foreign eqv |
| Courier services (Direct delivery to Beneficiary) | 0 |
| Open ended guarantees (charged per annum) | 3% p.a |
| Cancellation | TZS150000 or USD.64 or foreign eqv. |

| LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES | | |
|---|---|---|
| LOANS | CATEGORY | INTEREST RATE |
| Consumer Loans | Consumer Loan Administration Fee | 1.5% of the Approved loan. Minimum TZS. 10,000/= |
| Wastaafu Loans | Loan Application fee | TZS 10,000/= |
| | Loan Administration fee | 1.5% Minimum TZS. 10,000/= Maximum TZS. 100,000/= |
| Other Charges On Individual Micro Credit | MIC Loan Application fee | TZS 25,000/= |
| | MIC Loan Processing/ Administration fee | 1.5% Minimum TZS. 50,000/= |
| Interest Rates And Charges On Business Loan | Loan Application fee for Business and Personal loans | TZS. 50,000/= |
| | Loan Administration fee - Business and Personal loans | 1.5% of the Approved Amount. |

**Fanya miamala yako mahali popote, wakati wowote! Kujiunga bonyeza *150*21#**

**Head Office: 10th Floor - PSSSF Millenium Towers II, Bagamoyo Road, Kijitonyama, P.O Box 9300, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Telephone: +255 22 2162940, Email: info@tcbbank.co.tz | Website: www.tcbbank.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vyombo vya habari vihamasishe wananchi chanjo ya UVIKO-19

**VYOMBO** vya habari vina umuhimu mkubwa katika jamii, kiasi kwamba vimepewa hadhi isiyo rasmi kuwa ni 'mhimili wa nne wa dola'.

Hiyo inamaanisha kwamba vyombo vya habari ni muhimu sana baada ya Serikali, Bunge na Mahakama. Vyombo vya habari vina majukumu ya kuelimisha, kuburudisha, kutaarifu pamoja na kutengeneza ajenda.

Kutokana na majukumu hayo, jamii imejenga imani kwa vyombo vya habari, kiasi kwamba habari zinazotangazwa au kuchapishwa na vyombo hivyo zinaaminiwa na kila mwanajamii.

Umuhimu huo ndio unaosababisha vyombo hivyo kutumika katika kuripoti na kuhamasisha ushiriki wa jamii katika masuala mbalimbali yakiwamo ya maendeleo, maafa na mengine ambayo jamii inayatekeleza kwa wakati huo.

Kwa msingi huo, ndio maana hata mihimili mitatu ya dola hushirikisha kwa kiasi kikubwa vyombo vya habari kuripoti shughuli zake ili jamii ielewe kinachoendelea.

Kwa Tanzania, vyombo vyetu vya habari vimekuwa vikishirikishwa katika kampeni mbalimbali za kitaifa zinazohitaji uhamasishaji wa wananchi kushiriki kama uchaguzi mkuu, masuala ya afya kama chanjo, sensa ya watu na makazi.

Itakumbukwa jinsi vyombo vya habari vilivyoshiriki katika vita dhidi ya Nduli Iddi Amin wa Uganda, baada ya majeshi yake kuivamia Tanzania mwaka 1978, na hakika vilifanya kazi nzuri ya kuwataarifu kuhusu hatua mbalimbali za jeshi letu katika kuwaondoa wavamizi kwenye ardhi yetu pamoja na kuwahamasisha wananchi kutoa mchango wao wa hali na mali.

Hivi sasa dunia inakabiliwa na vita dhidi ya ugonjwa wa Covid-19, ambao uliingia nchini mwaka jana na kuambukiza watu kadhaa na wengine kupoteza maisha, huku serikali ikitangaza hatua mbalimbali za tahadhari kuepusha maambukizi. Pamoja na hatua hizo, Rais Samia Suluhu Hassan alikubali nchi yetu kukubali kuleta chanjo ili wananchi wachanjwe kudhibiti maambukizi na vifo, ambayo ilianza kutolewa mwishoni mwa Julai, mwaka huu.

Suala hili lina umuhimu mkubwa kwa taifa letu, hivyo vyombo vya habari vinakabiliwa na jukumu la kuihamasisha jamii ili wananchi wengi wajitokeze kupata chanjo hatimaye kufikia lengo la kuchanja idadi kubwa.

Katika kulipa uzito suala hilo, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji, juzi aliwataka wanahabari kuendelea kuwaelimisha Watanzania juu ya umuhimu wa kupata chanjo ya kuzuia maambukizi ya corona.


Alisema kwa kufanya hivyo, Taifa litakuwa sehemu salama dhidi ya maambukizi ya ugonjwa huo sambamba na kupunguza madhara yanayoweza kutokea.

Kama alivyosema Waziri Dk. Kijaji kuwa vyombo vya habari nchini vimekuwa mstari wa mbele kuripoti kuhusu ugonjwa huo tangu mwaka 2019, tunavisisitiza kuendelea kuwahamasisha Watanzania kuhusu chanjo, umuhimu wake kwa usalama wao na Taifa kwa ujumla.

Vyombo vya habari vijikite pia katika kuondoa upotoshaji unaofanywa na watu wachache kuhusu chanjo hiyo kwa maslahi yao binafsi. Sisi tunaamini kuwa chanjo ndiyo suluhisho katika mapambano dhidi ya tishio la corona.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Mwandishi Wetu

## Muungwana Lazima Nilonge

# Msajili na vyama, somo lenu 'hiloo'

**MKUTANO** wa vyama vya siasa, polisi na Msajili wa Vyama vya Siasa, uliokuwa ufanyike wiki iliyopita lakini ukaahirishwa ni fursa ya wahusika kutafakari njia zao na kuibua fikra kuhusu ofisi hiyo na vyama pia.

Unaweza kusema Ofisi ya Msajili kushindwa kukutana na vyama ikiwa ndiyo mlezi wa taasisi hizo za kisiasa unatoa picha kadhaa, kwanza, ni suala la uhusiano wake na wanae hao anaowalea.

Kunahitajika kuwe na uhusiano wa karibu na vyama vya siasa inavyovisimamia.

Pili inahitajika kuwa na ushawishi zaidi wa kuvileta pamoja vyama hivyo ambao ndiyo wadau wake.

Aidha, ushawishi huo ni muhimu ili kuboresha uamuzi ambao umekuwa na lawama kwenye kutafsiri sheria ya vyama vya siasa.

Inavyoonekana ina nguvu kisheria kuamua chochote kile, ikiamua kufanya jambo lolote inalitimiza bila kuzuiliwa.

Hata hivyo, inapaswa kuwa na wepesi kuruhusu mashauriano na vyama hivyo na wadau wengine ili kuwa na maridhiano.

Jambo jingine ambalo ni muhimu kwaofisi hii ni kuanza kuelewa kwa kina uhitaji wa vyama kwa sasa.

Ushauri huu ni muhimu kwavile inavyoelekea vyama kama CHADEMA, ACT Wazalendo na NCCR-Mageuzi vinahitaji kuonana na Rais Samia Suluhu Hassan na pengine siyo kikao hicho.

Ofisi hiyo imekuwepo kwa miaka mitano sasa ya sintofahamu baina ya vyama na serikali inafahamika. Kinachoendelea kwenye siasa ya vyama vingi nchini na kilio cha mikutano ya ndani kinajulikana.

Ofisi hii ishauriane na wadau mbalimbali ili isimame kutatua changamoto nyingi za vyama vya siasa.

Lakini, pia kuna malalamiko kama ya CHADEMA kuwa viongozi wake wana kesi na wapo mahakamani na wamekosa dhamana na wangetaka waachiwe ili kushiriki mkutano huo.

Kwa hiyo kunahitajika mijadala na mikakati ya kuweka mambo sawa kwasababu ajenda siyo kuzuiwa mikutano ya vyama vya upinzani, hata kesi pia. Wapinzani wanajiona kama majeruhi wa kisiasa.

Waliojeruhiwa kisiasa ni wengi kuanzia walioko mahakamani na magerezani hata vyama vingine kuvurugika.

Uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2019 na uchaguzi mkuu 2020 umeacha malalamiko na maswali mengi kwenye demokrasia ya vyama vingi nchini.

Ipo haja ya kuwa na mjadala mpana wa kitaifa kuhusu uchaguzi huo hasa kwenye kuwaengua wagombea wa upinzani kwa kutumia sababu nyepesi kama kukosea jina.

Lakini, pia kuna hoja za wabunge wa viti maalumu kuingia bungeni katika mazingira ambayo vyama vinayalalamikia.

Ndiyo maana pengine ni vyema ofisi hiyo ikatafakari zaidi na kuelekeza kipi cha kufanya kwavile kuja na mipango ya kuwakutanisha polisi na vyama vya siasa kunaonekana kuwa ni kukwepa lawama na kuwaangushia polisi jumba bovu la kisiasa.

Taifa lilipiga hatua kubwa miaka michache iliyopita kwenye masuala ya kidemokrasia na uhuru wa kisiasa lakini inavyoelekea linarudi tena nyuma.

Lakini vyama vya siasa navyo vinahitaji kujitafakari na kubadili mikakati yake kwa sasa.

Vikumbuke kuwa kususa mikutano na mlezi wake au Msajili wa Vyama siyo suluhisho kwa sababu majadiliano sio rahisi kuyakwepa kwa mazingira ya sasa.

Ni vyema nao kwenda mstari wa mbele kupambana kushiriki mijadala kwenye kila jukwaa wanalopata au kukaribishwa, walitumie iwe mikutano kama huo ulioitishwa na Msajili wa Vyama.

Vitumie pia vyombo vya habari au kushiriki kwenye uchaguzi wa aina yoyote unaokuja badala ya kulalamika.

Vyama visitegemee huruma za wananchi ambazo hazipo, vishiriki na viwe mstari wa mbele kushirikiana na wananchi, serikali, Ofisi ya Msajili badala ya kususa mambo.

## Ujerumani yaimwagia Tanzania bil. 190/-

**Na Benny Mwaipaja**

UJERUMANI imeipatia Tanzania msaada wa Euro milioni 71, sawa na Sh. bilioni 190.5 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Nyaraka za makubaliano ya msaada huo zilitiwa saini jijini Dar es Salaam kati ya Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango anayesimamia masuala ya Fedha za Nje, Amina Khamis Shaaban, na Kiongozi wa Ujumbe wa Serikali ya Ujerumani, Marcus Von Essen.

Akizungumza baada ya kutiwa saini kwa nyaraka hizo, Shaaban aliyataja maeneo yatakayonufaika na msaada huo kuwa ni afya ya mama na mtoto, iliyotengewa Euro milioni 24 na mradi wa kuzuia migogoro baina ya wanyamapori na binadamu, utakaotumia Euro milioni sita.

"Maeneo mengine yatakayonufaika na fedha hizi ni mpango wa kufidia upotevu wa makusanyo ya maduhuli katika sekta ya utalii kutokana na upungufu wa watalii walioingia nchini kwa sababu ya ugonjwa wa corona, kuzuia ujangili na kuboresha miundombinu kwenye makazi na jamii inayozunguka maeneo ya hifadhi za taifa, utakaogharimu Euro milioni 15," alisema.

Shaaban alisema Euro milioni 20 zitaelekezwa kuboresha huduma ya maji kwenye miji inayokua na Euro milioni tatu zitatumika kuboresha usalama wa maji kwenye maeneo ya baadhi ya miji nchini.

Alisema Euro milioni tatu zitatumika katika masuala ya kulinda haki za kinamama na wasichana wanaokabiliwa na ukatili wa kijinsia kwa kuwapatia msaada wa kisheria.

Shaaban aliishukuru Ujerumani kwa kuanzisha majadiliano na Tanzania baada ya kusitisha tangu mwaka 2015 na kuahidi kuwa fedha zitakazotolewa zitatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regine Hess, na Kiongozi wa Ujumbe wa Ujerumani ulioshiriki majadiliano hayo, Von Essen, walisema Ujerumani imeamua kufufua ushiriki katika kujenga maendeleo ya Tanzania ili kuunga mkono uongozi wa serikali ya awamu ya sita.

Walisema chini ya makubaliano mapya, Ujerumani itajikita zaidi kusaidia afya ya mama na mtoto, bima ya afya kupitia Mfuko wa Taifa wa bima ya afya (NHIF), maji na usafi wa mazingira, usimamizi wa fedha za umma, kuhifadhi maeneo ya urithi wa dunia kama vile hifadhi ya Selous na kuwalinda wanawake na wasichana dhidi ya vitendo vya kikatili.

Pia walisema Ujerumani itarejesha mipango yake ya kusaidia miradi ya maendeleo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na tayari imeanza kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa maji visiwani humo.

Walisema Ujerumani itatoa fedha zingine kesho na mikataba ya msaada kadhaa itatiwa saini ikiwa ni mwanzo mpya wa kuhakikisha kuwa Ujerumani inashirikiana na Tanzania katika kuwaletea wananchi wake maendeleo.

# Sabaya kizimbani tena kesi uhujumu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KESI ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wenzake sita inatarajiwa kuendelea leo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha kwa shahidi wa saba wa Jamhuri kutoa ushahidi.

Oktoba 22, mwaka huu, Ramadhani Juma, ambaye ni Ofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), alishindwa kutoa ushahidi mahakamani huko kwa madai kwamba aliugua ghafla.

Katika kesi hiyo, mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine ni: Silvester Nyegu (26); Enock Togolani (41); Watson Mwahomange (27); Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31) wanaokabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi.

Mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, Patricia Kisinga, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, aliomba mahakama hiyo kuahirisha kusikilizwa kwa shauri hilo kwa kuwa madai shahidi aliugua ghafla, hivyo asingeweza kupanda kizimbani kutoa ushahidi.

Katika kesi hiyo, shtaka la kwanza ni madai ya kuongoza genge la uhalifu linalowakabili washtakiwa wote, la pili ni kujihusisha na vitendo vya rushwa na linamkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake na tatu ni kujihusisha na vitendo vya rushwa linalomkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka, linamkabili Sabaya peke yake, akidaiwa kuwa Januari 22 mwaka huu, akiwa katika eneo la kwa Murombo jijini Arusha, alitumia vibaya nafasi yake ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, alimtisha Francis Mroso kumfungulia mashtaka ya kukwepa kodi.

Shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha na linawakabili washtakiwa wote saba, ikidaiwa kuwa Februari 22, mwaka huu, wakiwa katika eneo la Kwamurombo jijini Arusha, walijipatia fedha kiasi cha Sh. milioni 90, wakitambua kwamba kufanya hivyo lilikuwa ni zao la vitendo vya rushwa.




Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo (kulia), akimsikiliza Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, wakati wa hafla ya kukabidhi mabenchi ya kukalia wagonjwa na kabati ndogo za kuhifadhi vifaa vya wagonjwa waliolazwa hasa wajawazito na wanaojifungua katika Hospitali ya Mbagala Rangitatu vilivyotolewa na benki hiyo, jana. Kushoto ni Kaimu Mganga Mkuu wa Manispaa ya Manispaa ya Temeke, Dk. Martha Macha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibano TANESCO majibu hoja za CAG

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imetoa siku 72 kwa Bodi na Menejimenti ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kujibu hoja zilizoibuliwa kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20.

Aidha, imeagiza TANESCO kufuatiliwa madeni ya Sh. bilioni 238, ambayo inazidai taasisi mbalimbali na kuingia mikataba ya ulipaji wake.

Akizungumza jana na waandishi wa habari baada ya mahojiano na uongozi wa shirika hilo, Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka, alisema TANESCO imekuwa na matatizo mengi na kwa sasa menejimenti imebadilishwa, hivyo wamepewa muda zaidi wa kujibu kitabu cha CAG chenye kurasa 521.

"Kuna mambo mengi tumechukua machache mazito, ambayo tuliona tuwape na tumekubaliana nao ikifika Januari mwakani tukutane nao tuone haya tuliyowapa wamefikia wapi," alisema.

Alisema taarifa ya CAG imebainisha dosari kubwa kwenye hesabu za shirika hilo na kwamba kuna maeneo sita yenye dosari kubwa.

"Kuna usimamizi wenye dosari wa mikataba inayohusu moja kwa moja shughuli za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme, pia kuna mapungufu kwenye mikataba ya manunuzi mengine ya shirika, kuna mapungufu mbalimbali katika uandaaji wa taarifa za fedha, kuna dosari katika mifumo ya Tehama, dosari kubwa katika mifumo ya udhibiti wa ndani," alisema.

Alitaja dosari zingine zilizobainishwa na CAG ni upungufu wa utawala bora na usimamizi wa mali za shirika.

"Utawala bora ni kwamba kwa nini TANESCO imekuwa na mikataba haieleweki, kwa nini hawasimamii yale waliyokubaliana kwenye mikataba, yakafuatiliwa. Kwa nini unaambiwa ikifika kipindi hiki unalipa fedha kwa mtu aliyekuuzia umeme kama SONGAS hulipi na unajua itabeba riba, inawezekana ile mikataba imetengenezwa kwa maslahi ya mtu binafsi, kuna tatizo kwenye shirika kwa ujumla, hali ya madeni si nzuri.

"Kwa kuzingatia upungufu huo ambao umefafanuliwa kwa kina katika randama ya CAG yenye kurasa 521, kamati inaitaka bodi na menejimenti ya TANESCO kujibu kikamilifu hoja zote za CAG, kabla ya Januari 5, 2022,"alisema.

Alisema kamati hiyo itakutana na TANESCO mwezi huo kwa tarehe itakayopangwa, ili kutathmini kwa kiasi gani hoja za CAG zitakuwa zimefanyiwa kazi.

Kuhusu tatizo la kukatika kwa umeme, Kaboyoka alisema kwa mujibu wa majibu ya menejimenti mpya, tatizo hilo linatokana na mitambo kuwa ya zamani na wamejipanga kuhakikisha wanamaliza suala hilo.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema shirika hilo kwa sasa linakusanya madeni yote inayodaiwa na kudai.

"Deni ambalo TANESCO wanadai taasisi mbalimbali limefika Sh. bilioni 238 kwa hiyo zimetumia umeme, lakini bado zinadaiwa na shirika, tumeagiza wazifuatilie na waingie mikataba ya makubaliano ya namna ya kuhakikisha kwamba taasisi hizo zinalipa TANESCO, ili iendelee na majukumu yake,"alisema.

# Waziri aitwisha zigo ardhi Dodoma

**Na Munir Shemweta,**
DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amefanya ziara ya kushtukiza katika ofisi ya ardhi ya Jiji la Dodoma na kuagiza maombi 521 ya umilikishaji ardhi kukamilishwa ndani ya siku tatu.

Akiwa ameambatana na Katibu Mkuu wa Wizara, Mary Makondo, na menejimenti ya wizara, Dk. Mabula alisema pamoja na kuwapo changamoto, anachohitaji maombi 521 yawe yamekamilika katika kipindi cha siku tatu.

"Kuanzia sasa tunahitaji zile 'application' (maombi) zote ambazo hati zake watu wameomba zitoke ndani ya siku tatu. Kama ni kutoka saa nane za usiku tunahitaji hiyo kazi ikamilike ndani ya siku tatu," alisema.

Dk. Mabula aliwataka watendaji wa ardhi katika Jiji la Dodoma kuandaa hati zisizopungua 100 kwa siku moja sambamba na kuwataka kumhakikishia kwa maandishi ahadi walizompa katika kutekeleza maagizo yake.

Uamuzi wa Naibu Waziri wa Ardhi kufanya ziara ya kushtukiza ofisi ya ardhi unatokana na kujitokeza baadhi ya malalamiko ya ucheleweshaji umilikishaji ardhi kwa wananchi, jambo lililofanya wizara kuanza mkakati maalum wa ukwamuaji na uharakishaji utoaji hati kwenye jiji hilo.

Awali, Naibu Waziri na timu yake walitembelea vitengo vya ardhi katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma ili kubaini baadhi ya changamoto katika sekta hiyo.

Dk. Mabula alisema, Jiji la Dodoma ndiyo sura ya nchi hivyo maofisa wake wa ardhi wanatakiwa kuwapanga wananchi wanaokwenda kupata huduma kulingana na maeneo wanayotoka sambamba na maafisa hao kuvaa vitambulisho ili kutambulika kwa wananchi.

"Hatuhitaji kusikia kelele za watu hapa, ninyi mnachafua image ya wizara na sekta kwa sababu tu ya kutojipanga kwenye utendaji wenu wa kazi, mko wengi mnaweza kujipanga vizuri pamoja na kuwapo upungufu wa watumishi kwa baadhi ya maeneo," alisema Dk. Mabula.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mary Makondo, alieleza kuwa, wizara yake imejipanga kuhakikisha inaongeza kasi ya umilikishaji ardhi katika mkoa wa Dodoma na Maeneo mengine nchini.

Katika jitihada za ukwamuaji na kuongeza kasi ya utoaji hati katika Jiji la Dodoma, wizara yake imeamua kuongeza nguvu ya watumishi kutoka Makao Makuu ili kuharakisha kasi ya utoaji hati kwa wamiliki wa ardhi.

Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Amelye Chaula, aliweka wazi kuwa mwamko mkubwa umilikishaji ardhi kutoka kwa wananchi umesababisha ofisi yake kuelemewa na kazi.

Hata hivyo, alisema ofisi hiyo imekuwa ikifanya juhudi kubwa kuhakikisha wananchi wanapatiwa huduma kwa wakati pamoja na kuwapo changamoto kadhaa kwa baadhi ya maeneo hasa yale yaliyorithiwa kutoka iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) na kusisitiza kuwa maeneo mapya hayana changamoto ya umilikishaji.



Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Salome Mwandalanga (kulia), akisikiliza malalamiko ya mfanyabiashara wa duka la vifaa vya ujenzi wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi ya mlango kwa mlango inayoendelea mkoani Rukwa jana. **PICHA: TRA**

# Unyanyapaa watajwa kikwazo wanawake kugombea uongozi

**Na Julieth Mkireri,**
KISARAWE

IMEELEZWA kuwa unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu ni moja ya vitu vinavyochangia kundi hilo kushindwa kupata nafasi za uongozi wanapojitokeza kugombea, imeelezwa.

Hayo yamebainishwa jana mjini hapa wakati wa mdahalo wa nafasi ya mwanamke katika uongozi na siasa ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA).

Akizungumza katika mdahalo huo, Katibu wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) Wilaya ya Kisarawe, Ibrahim Tully, alisema moja ya vikwazo vinavyowakabili wanawake wenye ulemavu kuwa viongozi ni unyanyapaa.

Tully alisema wanawake wenye ulemavu wanaonekana hawajui kuongea chochote kwenye jamii, hivyo hata wanapogombea kukosa watu wa kuwaunga mkono.

"Kutokana na jamii kuwa na uelewa mdogo kuhusiana na wanawake wenye ulemavu kuwa wanaweza kuongoza, kundi hili limekuwa likikosa ujasiri hasa wa kuingia ulingoni kuchukua fomu na kugombea," alisema Tully.

Katibu huyo aliiomba TAMWA na taasisi zingine kuwajengea uwezo wanawake wenye ulemavu ili wathubutu kugombea nafasi za uongozi.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, alisema mdahalo huo ni sehemu ya pili ya mradi wa wanawake wanaweza ambao utakuwa unaeneza elimu ya kumwelezea mwanamke kuwa ni kiongozi na utahusisha vyombo vya habari.

Dk. Reuben alisema baadhi ya mila na desturi zinaeleza kuwa mwanamke ni wa kukaa nyumbani, hivyo viongozi wa dini na wa kimila wanatakiwa kusaidia kutoa elimu kuhusiana na mwanamke kuwa kiongozi.

Alisema tabia ya kutokuthubutu na kutokujiamini kwa baadhi ya wanawake inasababisha kuwaambukiza wengine wasigombee.

"Hiki ni kikwazo kingine kinachosababisha kutokuwa na idadi kubwa ya viongozi wanawake. Tubadilike ili tuwe mfano kwa wengine katika maeneo yetu kujitokeza na kugombea nafasi za uongozi," alisema.

Dk. Reuben pia alibainisha kikwazo kingine cha wanawake kushindwa kugombea nafasi za uongozi kuwa ni majukumu mengi katika familia.

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kisarawe, Eva Stesheni, aliwataka wanawake kuwa na mpango mkakati kwa wanaotaka kugombea ili uwaongoze katika safari ya kuwa viongozi.

# TPF yakanusha uvumi mgogoro

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Amani Tanzania (TPF) imekanusha kuhusika na taarifa za uvumi zikionyesha kutoelewana na Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Sadiki Godigodi.

Taarifa hiyo ilisambazwa kwenye mitandao ya kijamii kuanzia Oktoba 21, mwaka huu.

"Taarifa hizo ambazo zimesambazwa kwenye mitandao ya kijamii ikionekana kusainiwa na Mwenyekiti na ikiwa na mhuri unaoonekana wa taasisi, ni ya uongo pamoja na taarifa zingine zilizowekwa kwenye waraka huo," ilieleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo pia ilifafanua kuwa Taasisi ya Amani Tanzania inasisitiza ushiriki mzuri wa washiriki wake katika mkutano wake uliokuwa na kaulimbiu "Utekelezaji upya baada ya Covid: Je, Azimio la Sahara linawezaje kuchochea utulivu na utangamano wa Afrika?"

Mkutano huo uliofanyika Oktoba 16, 2021 jijini Dar es Salaam, unasisitiza umakini wake kwa kuheshimu hitimisho na mapendekezo yote yaliyoundwa kwa pamoja wakati wa mkutano uliotajwa hapo awali na Taasisi ya Mafunzo ya Amani na Migogoro (IPCS) na Taasisi ya Amani ya Tanzania (TPF) ya jijini Dar es Salaam.

Shirika la Amani la Tanzania limetangaza kwamba habari yoyote iliyotolewa, kwa jina la TPF, na kituo chochote cha media au mtandao wa kijamii iko nje ya wigo au yaliyomo taarifa hiyo ya sasa inapaswa kuzingatiwa kama habari bandia na haionyeshi mweleko wa TPF na kuridhika kwa washiriki kuhusu suala la Sahara.

HABARI KITAIFA

# PURA na washirika wajadili mradi gesi

Na Elizabeth Zaya

BODI ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) imekutana na kufanya kikao na viongozi wa kampuni za Shell na Equinor pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa niaba ya serikali kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa mradi wa kubadili gesi asilia kuwa kimiminika (LNG).

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Bodi ya PURA, Profesa Gasper Mhinzi, kikao hicho kilikuwa na nia ya kuwaongezea uelewa wajumbe wa bodi kuhusiana na mradi na manufaa yatakayotokana na utekelezaji wake.

"Katika kikao hiki kampuni hizi zimefanya mawasilisho mbalimbali yaliyokuwa na lengo la kutanua uelewa kwa wajumbe wa bodi na jinsi utakavyokuwa na manufaa kwa pande zote mbili yaani serikali ya Tanzania na wawekezaji," alisema Profesa Mhinzi.

Profesa Mhinzi alisema kuwa kikao hicho kilijikita katika kuuelewa mradi kwa undani ili kuboresha utekelezaji wake.

Naye Makamu wa Rais na Mwenyekiti Mkazi wa Shell, Jared Keuhl, alisema kuwa ni muhimu kwa wadau wote ikiwamo serikali na wabia wa mradi kushirikiana na kuhakikisha katika hatua hizo za mwisho za maandalizi ya mradi kunakuwa na uwazi wa kutosha katika maamuzi yanayofanyika.

"Japokuwa hatua tuliyopo inaelekea ukingoni ni vizuri kila kitu kifanyike kwa ufasaha na uwazi mkubwa katika kipindi chote, na japokuwa majadiliano haya ni ya kuangalia maslahi ya pande zote mbili tunatamani yawe majadiliano ya ushirikiano," alisema Keuhl.

Kikao hicho ni mwendelezo wa maandalizi ya majadiliano ya HGA baina ya serikali na wabia wa mradi wa LNG yanayotarajiwa kuanza rasmi Novemba 8, 2021.

Mradi wa LNG ambao utasimamiwa na PURA unakadiriwa kuwa wa thamani ya takriban Dola za Marekani bilioni 30. Unatarajiwa kutengeneza ajira 6,000 za moja kwa moja na zaidi ya 15,000 zisizo za moja kwa moja kwa Watanzania.

# Alalamika kusuasua uchunguzi wa mauaji ya mwanawe Kibiti

Na Maulid Mmbaga

MKAZI wa Kijiji cha Msindani Kata ya Mwambao Wilaya ya Kibiti mkoani Pwani, Burhani Jadidi, baba mzazi wa Ayubu Jadidi (36), amelalamika akidai kutopata ushirikiano kutoka kwa polisi baada ya mwanawe kuuawa na anaodai kuwa ni wafugaji.

Akizungumza na Nipashe jana ofisi za gazeti hili, alisema mwanawe Ayubu alikuwa ni mkulima na Agosti 30, mwaka huu akiwa shambani kwake majira ya jioni alivamiwa na watu aliodai kuwa ni wafugaji na kumuua kikatili kwa kumkata na mapanga.

Alisema baada ya tukio hilo na kufanikiwa kuutambua mwili wa ndugu yao walitoa taarifa kwa polisi Kibiti ambao alidai kwamba walifika eneo la tukio siku ya pili na kutoa ruhusa kuwa mwili uzikwe huku wakiwaomba wanafamilia kuwa watulivu kwani hatua zitachukuliwa dhidi ya wauaji.

"Baada ya kuzika hatua zimekuwa kinyume chake hadi sasa hatujapatiwa ufumbuzi licha ya familia kutoa ushirikiano mkubwa kwa polisi kwa kuwataja watuhumiwa wetu kuwa ni wafugaji waliopo katika maeneo yetu ya mashamba, ambao tumekuwa tukizozana nao mara kwa mara kwa kupitisha mifugo katika mashamba yetu na kuharibu mazao, huku wakikaidi na kutishia kutupiga kama tutaendelea kuwakataza.

"Pamoja na wafugaji hao, wapo viongozi wa wafugaji na viongozi wa kata na kijiji bado wanawalinda wafugaji na kusababisha sheria isichukuliwe dhidi ya watu tunaowatuhumu kwa kuwakingia kifua wasikamatwe," alisema Jadidi.


Aliongeza kuwa hana imani na viongozi wake wa kijiji kwa madai kuwa wanaonekana kuwa upande wa watuhumiwa kwa kuwatetea wasikamatwe kwa maslahi yao binafsi, kitu alichodai kuwa hawatendewi haki.

"Mwenyekiti wa kijiji pamoja na kiongozi wa wafugaji kulikuwa na umuhimu wa kuhojiwa na polisi, kwani walikiri kupokea taarifa kwa njia ya simu siku ya mauaji, huku mashambani katika kijiji chao kuna mauaji yanatekelezwa na wafugaji dhidi ya mkulima.

Kamanda wa Polisi Kanda ya Rufiji, John Malulu, alithibitisha kupokea taarifa hizo za mauaji, na kusema upelelezi umebaini kwamba siku chache kabla marehemu hajafikwa na umauti kulikuwa na mgogoro kati yake na mtuhumiwa ambaye hajatiwa nguvuni.

Alisema ilichukua muda polisi kupata taarifa kuwa kuna tukio la mauaji limetokea, na hadi sasa hawajapata shahidi ambaye alikuwapo katika tukio na anayeweza kutoa maelezo ya kutosha ili kukamilisha upelelezi, kwani tukio lilitokea porini.

"Wanaosema kuwa upelelezi unasuasua sio kweli, upelelezi unaendelea na presha tunayoipata kutoka kwa familia ya marehemu inataka tukamate watu wote, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa upelelezi, hivyo waendelee kuwa na subira kwani uchunguzi unaendelea," alisema Kamanda Malulu.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Mwigulu Nchemba (watatu kushoto), akikabidhi mfano wa Hundi ya thamani ya Sh. bilioni 7.6 kama gawio kutoka benki ya CRDB kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba, aliyeongozana na Mkurugenzi wa Fedha, Beatrice Musa-Lupi (wapili kushoto) na Maofisa Uhusiano waandamizi wa Mfuko. Wakwanza kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya benki ya CRDB, Ally Hussein Laay na wakwanza kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo , Abdulmajib Nsekela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PSSSF yapokea gawio la bil. 7.6/- kutoka CRDB

Na Mwandishi Wetu

MFUKO wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), umepokea gawio la zaidi ya Sh. bilioni 7.6 kutokana na uwekezaji wa hisa katika Benki ya CRDB.

Hafla ya kukabidhi gawio kwa Serikali Kuu na Taasisi za Umma kutokana na faida ambayo benki ilipata mwaka 2020 ilifanyika juzi jijini Dar es Salaam ambapo mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ambaye alizipongeza taasisi za umma kwa uwekezaji huo ambao umeleta tija.

"Niwapongeze kwa kweli wanahisa, huu ndio utaratibu wa kuendesha uchumi kwa njia za kisasa, mnachokifanya kinaangukia kwenye sifa za uendeshaji wa uchumi wa kisasa," Alisisitiza Waziri Nchemba.

Mkurugenzi wa Fedha wa PSSSF, Beatrice Musa-Lupi, alisema Mfuko unayo furaha kubwa kuona kwamba uwekezaji huo umeleta faida kwa wanachama.

"Uwekezaji huo unafanywa kwa kuzingatia sheria iliyoanzisha Mfuko ambayo inatoa wajibu wa kukusanya michango na wajibu wa kuwekeza ili kulinda thamani ya michango ya wanachama na kuleta uwajibikaji katika kulipa Mafao," alifafanua Lupi.

Alisema Mfuko unapofanya uwekezaji huangalia misingi ya uwekezaji kwa kuangalia mahala ambapo ni salama na CRDB ni moja ya maeneo salama ambapo hisa za Mfuko ziko salama na zinaleta faida. Alitolea mfano mwaka 2019 ambapo Mfuko ulipata gawio la Sh. bilioni 5.8 na mwaka 2020 gawio limeongezeka na kufikia Sh. bilioni 7.6.

Alisema Mfuko utaendelea kuwekeza maeneo mengine, ambayo ni salama na yanayoleta faida na kuchochea uchumi kwenye taasisi hizo ziwe zinazofuata taratibu za nchi kama ulipaji wa kodi.

"Mfuko utaendelea kufuata vigezo vyote na sheria inavyoelekeza kuhakikisha kuwa fedha tulizowekeza ziko salama, zinaleta faida, lakini pia zinachangia katika ujenzi wa uchumi wa taifa letu," alisisitiza Lupi.

# Bodaboda 1,300 wapewa vifaa vya usalama, mbinu kudhibiti uhalifu

**Na Cristina Mwakangale**

ZAIDI ya madereva 1,300 wa pikipiki na bajaji jijini Dar es Salaam, maarufu kama bodaboda wamepewa mavazi maalum yanayoakisi mwanga (reflectors) kwa ajili ya kujihakikishia usalama wao hasa nyakati za usiku.

Kadhalika, wamehamasishwa kuzingatia sheria ya usalama barabarani kuepuka vifo na majeraha. Bodaboda hao wamekabidhiwa vifaa hivyo vilivyotolewa na kampuni ya michezo ya kubahatisha ya 22Bet, wakati wa mkutano kati yao na uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam uliowakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ndatwa Ludigija, Mkuu wa Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani wa mkoa huo , Abdil Issango na viongozi wengine.

Akizungumza wakati wa mkutano huo, Mkuu wa Wilaya aliwataka madereva hao kutumia vifaa hivyo ipasavyo, kuzingatia sheria za barabarani pamoja na kuepuka vitendo visivyofaa vinavyoweza kusababisha ajali za barabarani.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya alieleza kuwa ili kuepuka vitendo vya kihalifu na changamoto nyingine, ni vyema vikaanzishwa vituo tambuzi vitakavyokuwa na idadi maalum ya madereva ambao watapewa namba kama ilivyo kwa madereva taxi.

"Kwa kuweka vituo tambuzi ambavyo vitakuwa na idadi husika ya madereva, itapunguza kwa kiasi kikubwa vitendo vya kihalifu ambavyo vimekuwa vikifanywa na baadhi ya madereva bodaboda wasio waadilifu," alisema Ludigija.

Kiongozi huyo aliiagiza Halmashauri wa Manispaa ya Ilala kushirikiana na uongozi wa bodaboda, TARURA, na Jeshi la Polisi kuhakikisha wanakamilishi ujenzi wa vituo hivyo na kuwasihi madereva hao kuviheshimu vituo hivyo pindi vitakavyo kamilika.

Naye Kamanda Issango aliwataka madereva hao kuhakikisha wanatoa ipasavyo reflectors), kuvaa kofia ngumu, kuepuka kupakia abiria zaidi ya mmoja na kuhakikisha abiria pia amevaa kofia ngumu.

Mwenyekiti wa bodaboda Mkoa wa Dar es Salaam, Said Kagomba, aliishukuru kampuni ya 22Bet kwa kujitolea kuwapa vitendea kazi, pamoja na uongozi wa mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwamasisha na kuwapa elimu ya usalama barabarani pamoja na jinsi ya kuepuka uhalifu.



Mkuu wa Wilaya ya Temeke, mkoani Dar es Salaam, Jokate Mwegelo (wa pili kulia), akiwa na wanafunzi wa Shule za Msingi za Madenge na Ruvuma, pamoja na maofisa kutoka TARURA na taasisi isiyo ya kiserikali ya Amend wakati akikata utepe kuzindua alama za usalama barabarani katika shule hizo zilizotengenezwa na taasisi hiyo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kesi ya anayedaiwa kutorosha wanafunzi yapigwa kalenda

**Na Thobias Mwanakatwe,** MBEYA

KESI inayomkabili mfanyabiashara wa mjini Kyela, Bush Mwalusako, ambaye anayeshtakiwa kwa makosa ya kubaka na kutorosha wanafunzi wa sekondari kwa zaidi ya miezi nane imepigwa kalenda hadi Novemba 22, mwaka huu.

Kesi hiyo namba 40 ya mwaka huu ambayo ipo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, imeahirishwa jana kufuatia mtuhumiwa kushindwa kufika mahakamani kutokana na kuugua.

Wakili wa mshtakiwa huyo, aliieleza mahakama kuwa mteja wake anaumwa, hivyo kuiomba mahakama kupanga tarehe nyingine kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Kufuatia ombi hilo, Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Mbeya, Andrew Peter Scout, aliamua kuiahirisha hadi Novemba 22, mwaka huu. Mtuhumiwa yupo nje kwa dhamana.

Mfanyabiashara huyo kabla ya kukamatwa mwishoni mwa Agosti mwaka huu na kufikishwa mahakamani, alikuwa akitafutwa kwa zaidi ya miezi minane hadi alipokamatwa eneo la mpaka wa Namanga mkoani Arusha akiwa na mwanafunzi mmoja ambaye ni kati ya wawili aliokuwa akituhumiwa kuwatorosha.

Wanafunzi hao wanadaiwa kutoroshwa Januari mwaka huu.

# Wabunge waridhishwa uwekezaji kiwandani

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria imewataka wawekezaji na wafanyakazi wa kiwanda cha kimataifa cha bidhaa za ngozi Kilimanjaro (KLICL) kufanya kazi kwa juhudi, weledi na maarifa ili makusudio ya kuanzishwa kwa kiwanda yafikiwe.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Kaimu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Najma Murtaza Giga wakati wa ziara ya kamati katika kiwanda hicho , kilichopo mjini Moshi mkoani Kilimanjaro.

"Kamati itaendelea kusimamia na kushauri ili kiwanda kiwe endelevu kwa maslahi ya wananchi kwa ujumla," alisisitiza Giga.

Giga aliwataka watumishi wa kiwanda kuwa wabunifu na waaminifu katika kulinda miundombinu ya kiwanda ambacho ni mali ya Watanzania wote.

Wajumbe waliipongeza mipango ya kiwanda hicho na kushauri kilenge kuwa na viwango vya kimataifa ambapo pia walipongeza kutoa ajira kwa Watanzania wengi wakiwamo vijana na wanawake, huku kamati ikishauri elimu zaidi itolewe juu ya bidhaa za kiwanda hicho na maduka yasambae nchi nzima.

Mjumbe wa kamati hiyo na Mbunge wa Chonge, Salum Saffi, alishauri kiwanda hicho kujipanga kuwa na wataalam wazawa na kuachana na tabia ya kutegemea wageni katika uendeshaji wake.

Naye Omary Omary alisema: "Kwa upande wangu nimeshaanza kutumia bidhaa za kiwanda hiki, naomba kiwanda kilenge kuzalisha bidhaa bora za viwango ili kupata soko la uhakika, hasa kwa soko la Zanzibar."

Mbuge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo, alisema: "Wana Moshi wapo tayari kulinda kiwanda hicho. Pia nashauri ili tuweze kupata soko la uhakika la bidhaa za kiwanda hiki, tuhakikishe bidhaa zilizo chini ya viwango haziruhusiwi kuigizwa nchini."

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), Patrobas Katambi, alishukuru kamati hiyo kwa kutembelea kiwanda na kusema hoja zote zimepokelewa na zitafanyiwa kazi vyema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda hicho, CPA. Hosea, alisema wataalamu kutoka nje waliopo kiwanda wanatoa elimu kwa watumishi Watanzania kwa kila hatua ili waweze kuendesha vilivyo kiwanda wakati wote.

"Wataalamu waliopo kiwanda wanafunga mashine mbalimbali, tumekubaliana watumishi wa Kitanzania wahusike katika kila hatua ili waweze kupata ujuzi na hatimaye kiwanda tukiendeshe wenyewe" alisema Mwenyekiti huyo ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF). Nae Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda, Mhandisi Masud Omari, alisema kiwanda kimeanza uzalishaji wa bidhaa mbalimbali za ngozi kama; viatu vya kike na kiume, viatu vya shule na viatu vya majeshi yote nchini.

"Tumeaza uzalishaji, hivyo tunatoa wito kwa Watanzania wote kuvaa viatu vya kiwanda chetu, kwani ni bora na imara na vinapatikana kwa bei nafuu" alisisitiza Mhandisi Omari.

Kiwanda cha bidhaa za ngozi kinamilikiwa kwa ubia kati ya Jeshi la Magereza na PSSSF.

## MWANASIASA AFUNGUKA…

Si kinamama pekee wanaume pia tunanyanyaswa kijinsia



Ukurasa 12

**siasa**

JUMATANO OKTOBA 26, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Ukurasa 14

**Wakuu mikoa, wilaya wasaa wa manispaa mpya ni sasa**

## MKUTANO MSAJILI VS VYAMA

# Ndiyo ushauri wa wadau kufanikisha kikao Desemba

**Na Sabato Kasika**

MKUTANO kati ya Msajili wa Vyama vya Siasa, viongozi wake na Jeshi la Polisi unatarajiwa kufanyika tena Desemba mwaka huu, baada ya ule wa Oktoba 21, kukwama.

Hatua hiyo inafuatia kuahirishwa kwa mkutano huo uliokuwa umegubikwa na sintofahamu wakati wote, kutokana na kile kilichoelezwa kuwa ni kutoa nafasi kwa ajili ya wadau wengi zaidi kushirikishwa.

Maelezo hayo ni ya Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa Tanzania, Juma Ali Khatib, anayezungumza na vyombo vya habari hivi karibuni na kwamba kinachosubiriwa ni tarehe.

Baada ya kuahirishwa kwa mkutano huo, baadhi ya wachambuzi na wadau wa siasa wanatoa maoni na mitazamo yao kuhusu hatua hiyo na kile wanachoamini kwamba kinaweza kuufanikisha mwingine unaokuja.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene. **PICHA: MTANDAO**

### KUONGEZA WASHIRIKI

Mchambuzi wa masuala ya siasa kutoka Dar es Salaam, Said Msonga, anasema, kuna haja ya kuongeza wadau zaidi wa mkutano huo, ili kupanua wigo wa kile ambacho kimepangwa kujadiliwa ili hatimaye kuleta mwafaka wa kudumu.

Anashauri kuwa kuanzia sasa hadi Desemba, muda huo utumike kualika washiriki wengine wanaokusudiwa kwenye mkutano huo badala ya kuacha uwe wa msajili, polisi na viongozi wa vyama vya siasa tu.

“Ninashauri hivyo kwani msajili kwa upande wake amekuwa akishutumiwa huenda kwa kutotimiza wajibu inavyopasa, polisi nao wanalaumiwa kuwa wananyanyasa upinzani, nani hakimu hapo?” Anahoji Msonga.

Anasema, kwa mazingira kama hayo, wanahitajika wawepo wadau wengine zaidi, ambao watasaidia kupatikana kwa muafaka badala kuacha wale wanaotuhumiwa ndiyo wasimamie mkutano.

“Washirikishwe wengine kama Baraza la Vyama vya Siasa, Kituo cha Demokrasia, Idara ya Siasa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Jukwaa la Katiba, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Waziri wa Sheria na Katiba na taasisi huru za kiraia,” anasema.

Mchambuzi huyo anasema, huenda mazuio ya mikutano ya hadhara kwa vyama vya siasa yamesababisha wananchi wakose haki kupata taarifa mbalimbali na kuzimua maamuzi.

“Lakini pia, wananchi hupata taarifa mbalimbali za kisiasa na nyingine kupitia vyama na asasi za kiraia, pamoja na hayo, chama tawala kinaweza kujitathmini na kujirekebisha kwa kukosolewa vyama vya siasa,” anasema.

### MKUTANO ILI NINI?

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anasema haoni umuhimu wa mkutano huo, kwa madai kwamba kinachotakiwa ni kuzingatia, katiba na sheria.

“Kila kitu kipo kisheria, kwani polisi na wanasiasa wana ugomvi hadi msajili awakutanishe? Sioni umuhimu wa kuwapo kwa mkutano huo bali katiba na sheria vifuatwe,” anasisitiza Dk. Helen

Anasema, katiba na sheria vikisimamiwa kikamilifu hakutakuwapo na sintofahamu kati ya polisi na vyama vya siasa ambayo inamfanya msajili kuitisha mkutano kati yake, polisi na viongozi wa vyama hivyo.

“Ninaamini kuna tatizo ambalo bado hajalishughulikiwa, la kuacha polisi wakizuia mikutano hata ya ndani ya vyama vya upinzani, wakati chama tawala kikiendelea na shughuli zake bila kunyooshewa kidole,” anasema.

Dokta Helen anasema, badala ya kuitisha mkutano, polisi waelekezwe kufanya kazi kwa mujibu wa sheria, na kwamba hatua hiyo inaweza kusaidia shughuli za kisiasa kufanyika bila kuingiliwa au kulalamikiwa.

“Kuahirishwa kwa mkutano wa awali kulikuwa hakukwepeki, hasa kutokana na ukweli kwamba, vyama ambavyo vinaathirika zaidi nauamuzi wa kuzuiwa kutokana na kuzuiwa kwa mikutano ya hadhara vilisusa,” anasema.

Mwanasheria huyo anasema, hata kama ungefanyika, usingekuwa na uamuzi ambao ungesaidia kushawishi vyama ambavyo anadai vimeathirika na utaratibu wa kuzuia kuuendesha shughuli za kisiasa.

Kabla ya kuahirishwa na kupangwa upya, baadhi ya vyama vilikuwa tayari vimegawanyika, vingine vikiwa vimesusia mkutano huo na baadhi vikiwa vimekubali kushiriki katika mkutano huo.

Vyama vilivyokuwa vimezungumza na gazeti hili na kuthibitisha kushiriki mkutano huo vilikuwa ni Chama cha Alliance Democratic Change (ADC) na Chama cha Wananchi (CUF).

Katibu Mkuu wa ADC, Doyo Hassan Doyo, alisema, meza ya mazungumzo ndiyo huleta muafaka, hivyo hakuona ni kwa nini chama chake kisihudhurie mkutano huo muhimu kwa ajili ya demokrasia ya vyama vingi nchini.

CUF kwa upande wake ilijipanga kuhudhuria ikiwa na ajenda kadhaa ikiwamo kutaka ufafanuzi wa kina kuhusu vyama vya siasa kuzuiwa kufanya mikutano ya hadhara kwa zaidi ya miaka mitano.

Ajenda nyingine ilikuwa ni kutaka kujua ni kwa nini polisi wanavamia vikao vya ndani vya vyama na pia kufahamu sababu za viongozi wa vyama vya upinzani kukamatwa ovyo na kuwekwa ndani.

Kwa mujibu wa Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Bara, Magdalena Sakaya, Msajili anatakiwa kuhakikisha vyama vinakua na kushamiri na kwamba hilo limekuwa kinyume.

### KUSUSA MKUTANO

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kilitangaza kususa mkutano na kutoa masharti kwa msajili ambayo kilitaka yatelekezwe kwanza ndipo kiangalie uwezekano wa kushiriki.

Miongoni mwa masharti hayo yalikuwa ni kutaka msajili huyo aruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, kuachiwa huru bila masharti mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe.

Sharti jingine lilikuwa ni kutaka wanachama wa chama hicho ambao ni wafungwa wa kisiasa na wengine waliowekwa mahabusu, katika magereza mbalimbali nchini, waachiwe huru.

NCCR MAGEUZI walisusa kuhudhuria kwasababu za kutoshirikishwa katika maandalizi, kutokuwepo kwa uwazi, na kwamba watuhumiwa hawawezi kujipa kazi ya unyapara na usuluhishi.

Wanadai kuwa hakuna mahali Msajili wa Vyama ametekeleza wajibu wake wa kisheria na kuongeza kuwa mkutano huo haukuwa na nia njema, bali kufifisha na kubeza hoja zao halali za kuhakikisha taifa linakuwa na mfumo imara na wenye utu.

Kwa upande wa Chama cha ACT- Wazalendo, wao walikuwa kwenye vikao vya kujadili wahudhurie au wasishiriki mkutano huo, lakini baadaye wakapata taarifa za kuahirishwa kabla hawajafikia mwafaka.



Mohamed Bushir, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Mbopo, Mabwepande, akielezea yaliyomsibu akisaka uongozi wa kisiasa. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

MWANASIASA AFUNGUKA…

# Si kinamama pekee wanaume pia tunanyanyaswa kijinsia

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI wa kuwania uongozi, viongozi wanaoshinda na wanaoangushwa wana mengi ya kusimulia kuanzia visa mkasa vya kusisimua hadi unyanyasaji na udhalilishaji unaojipambanua kwenye mfumo wa dume.

Wenye simulizi wanasema wagombea kupata nafasi za uongozi kwenye mashina kuna vikwazo vingi achilia mbali jamii kudhani kwamba kinamama pekee ndiyo wanaokumbana navyo. Hata wanaume wananyanyaswa na kunyanyapaliwa pia.

Mohamed Bushir, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mbopo, mkoani Dar es Salaam, anasimulia aliyoyapitia kabla kupata nafasi hiyo, akipachikwa majina tofauti ya kumdhalilisha.

Anasema kupata uongozi ngazi ya chini, ikiwamo mtaa kuna changamoto nyingi kwa wanawake na wanaume, akisema elimu inahitajika ili jamii itenganishe dhana potofu na uongozi.

"Binafsi najishughulisha na kazi za saluni za wanawake, nilikuwa na saluni yangu siku nyingi kabla hata sijafikiria kugombea uenyekiti, ni msusi hodari kazi inayoniingizia kipato cha kuendesha familia yangu.

"Nilipochukua fomu kugombea uenyekiti maneno yaliibuka mengi, kwamba mimi ni shoga, msimchague huyo shoga atuongoze," anaeleza.

Bushir, anazungumza hayo katika mafunzo yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), yakikutanisha wenyeviti wa mitaa, watendaji kata na madiwani wa Mabwepande.

> "Mfumo dume, mawazo mgando yalinifanya niache kazi, ila nimekaa nikafikiria nimeamua nitairudia shughuli yangu niliyoipenda," anasema...

Anasema mfumo dume upo katika makundi yote na kuathiri wanaume na kinamama, tofauti na jamii kuamini kwamba mfumo huo watendaji wakuu ni wanaume.

"Mfumo dume, mawazo mgando yalinifanya niache kazi, ila nimekaa nikafikiria nimeamua nitairudia shughuli yangu niliyoipenda," anasema Bushir.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Vaileth Kabigumi, katika mafunzo hayo, anasema ripoti zinazofika ofisini kwake zinazohusu masuala kijinsia zinatoka kwa wanawake, licha ya kwamba kuna wanaume pia wanaotendewa vitendo hivyo.

"Mfumo dume upo pande zote na unaathiri kila jinsi. Matukio yanayoripotiwa zaidi kuhusu ukatili wa kijinsia ni wanawake, lakini wapo wanaume anakumbwa na hali hii, kutokana na mila, desturi ni vigumu mwanaume kuripoti.'

William Chitanda, Mwenyekiti wa serikali ya mtaa Michungwani Kata ya Saranga, anasema ripoti kuhusu ukatili wa kijinsia zipo mtaani kwake hasa zinazohusu ndoa.

"Migogoro ya ndoa ipo zaidi, chanzo nyingi ni udhalilishaji kijinsia, jamii bado inahitaji kupewa elimu kuachana na hayo," anasema Chitanda.

KUPATA ELIMU

Deogratius Temba, mwezeshaji wa masuala ya kijinsia anaelezea namna dhana tofauti kwenye jamii ambazo zimezoeleka na kurithiwa na kusababisha vikwazo vya maendeleo kijamii bila jamii husika kubaini tatizo hilo.

Anasema ipo mikataba ya kikanda na kimataifa, ambayo ina uhusiano na masuala ya kijinsia, ikiwamo Mkataba wa Umoja wa Afrika (AU) wa Haki za Binadamu na Wanawake 2003, Sera ya Jinsia na Maendeleo ya Jumuiaya ya Afrika Mashariki (EAC), pamoja na Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu 1948.

Mengine ni Azimio la Mpango Kazi wa Beijing, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), mkataba wa kutokomeza aina zote za dhuluma na ukataili dhidi ya wanawake 1979 pamoja na Agenda 2063 Afrika Tunayoitaka 'Africa we Want'.

"Katika jamii kuna dhana nyingi zinazoathiri pende zote. Hata wanaume wanakumbwa na matukio ya ukatili ila hawaripoti kokote, linaishia moyoni. Hii inawaathiri kwa moja au jamii. Wanabaki na hasira, msongo wa mawazo na visasi kwavile hawana pa kuitoa sumu hiyo.

"Kwenye jamii tunaamini kwamba mawaume ni jasiri, shupavu anaweza kila kitu lakini. Kusema anakumbana na ukatili wa kijinsia ni ngumu, atabaki kupambana na nafsi yake."

Temba anasema kwenye mikoa mingi ambayo wameifikia katika kutoa elimu kuhusu masuala ya kijinsia walibaini kuna ugumu wa wanawake wanaowania nafasi mbalimbali kuanzia ngazi ya chini kuanzia mashinani na kata.

Anasema ugumu huo unatokana na mfumo dume, mawazo mgando na mgawanyo wa majukumu ya kijinsia kwenye jamii inasababisha baadhi kuamini kwamba kazi ya uongozi ni kwa wanaume pekee.

"Mawazo mbadala ni muhimu ili kuwaweka kwenye mstari. Mila na desturi zinasababisha kuwapo mawazo mgando kwamba kazi hii ni ya mwanamke, mwaume, wenzetu nchi zilizoendelea wamepiga hatua kwa sababu ya iongozi kuwa shirikishi kwa makundi yote na kutoa fursa.

"Baadhi ya maeneo wanadhani haiwezekani mwanamke kuwa dereva, kuna madhara ya kimaendeleo kutokana na mfumo dume mawazo mgando, sera, sheria kandamizi ambazo tumejiwekea sisi wenyewe," anasema Deogratius.

**HALI HALISI**

Diwani wa Viti Maalumu Liberatha Samson anasema manispaa ya Ubungo mkoani Dar es Salaam ina madiwani wanawake sita kati 19 huku wenyeviti wa mitaa wakiwa wanne kati ya 90.

Aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro na Diwani wa Kata ya Ngerengere, Kibena Nassoro, anasema mkakati wa wanawake ni kuhakikisha kuwa ifikapo 2025, idadi ya wenyeviti kwenye halmashauri inaongezeka.

Kibena ambaye pia alikuwa mwenyekiti wa Wanawake wa Serikali za Mitaa (WASEMI), anasema watandelea kuhamasisha wanawake kujitokeza kugombea na kushinda, bila kukata tamaa.

# Elimu, uwezeshwaji kiuchumi, lilivyo hitaji muhimu kufikia 50/50

**Na Reubeni Lumbagala, DODOMA**

OKTOBA 15 duniani kote inaadhimishwa 'Siku ya Mwanamke wa Kijijini' na Umoja wa Mataifa (UN), umeridhia tarehe hiyo kutengwa maalum kutafakari mchango wa mwanamke wa kijijini, changamoto zake na namna bora ya kuzitatua ili kumjengea ustawi na maendeleo kwa kuangalia kazi zake.

Mwaka huu , maadhimisho yana kaulimbiu "Ardi ni Nyenzo kwa Maendeleo ya Mwanamke wa Kijijini".

Kwa miaka mingi, kutokana na uwepo wa mila na desturi kandamizi, wanawake hasa wa vijijini wamekuwa wahanga wa kutoshirikishwa kwenye masuala ya kimaendeleo.

Kutokana na mila na desturi za kubagua wanawake, unyanyasaji wa kijinsia, mila kandamizi kwa kiasi kikubwa zinaendelea kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Zama hizi kutokana na utandawazi na mabadiliko ya kisera ya kidunia, wanawake wamekuwa wadau muhimu katika ushirikishwaji wa masuala ya kimaendeleo katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii lengo likiwa ni kufikia uongozi wa 50/50.

Pamoja na uwepo wa matatizo mengi kwa kinamama wa vijijini, elimu na uwezeshwaji kiuchumi ni nyenzo muhimu ya kuwasaidia kupiga hatua kimaendeleo, kuanzia kisiasa, uchumi, uongozi na kuondoa ukandamizwaji.

Elimu ni msingi wa maendeleo, hivyo jamii inapaswa kuunga mkono juhudi za serikali za kusomesha watoto wote wasichana kwa wavulana bila ubaguzi. Mtazamo na dhana potofu kuhusu wasiwasi wa uwezo wa wasichana kumudu masomo unapaswa kubadilika, ili wasiachwe na wapate fursa sawa na wavulana katika kupata elimu. Dhana ya kutaka wasichana waolewe na kutunza familia bila kujali haki zao za msingi kama elimu iondoke sasa, ndiyo maana wanaharakati wanaanza kulitaka bunge kuanza mchakato wa kubadilisha sheria ya ndoa ya 1970 inayoruhusu msichana wa chini ya miaka 18 kuolewa.

Kuwanyima nafasi ya kusoma kunawakatili wasichana malengo yao ya kupata elimu, hivyo basi, mabinti wapewa elimu, kwani ni dhahiri jamii itakuwa na kundi kubwa la wanawake walielimika na wenye uwezo wa kumudu maisha yao na familia zao kwa mafanikio kuliko ilivyo sasa.

Taifa haliwezi kusonga mbele kimaendeleo kama wasichana na wanawake hawatapewa kipaumbele na fursa sawa katika sekta ya elimu na nyingine muhimu.

Nchi inahitaji rasilimaliwatu ya kutosha yenye ujuzi, maarifa na stadi mbalimbali ili watumike kuleta maendeleo, hivyo, ni muhimu wasichana na wanawake ambao ni kundi muhimu na kubwa katika taifa hili wakawa sehemu ya maendeleo kwa kupata elimu bila ubaguzi wowote.



Kinamama vijijini wana mchango mkubwa wa maendeleo kuanzia kilimo, ufugaji na biashara. **PICHA: MTANDAO.**

Kiuchumi; uwezeshwaji wanawake katika kumiliki ardhi ni muhimu kwa wanaokaa vijijini, hii ni kutokana na ukweli kuwa shughuli zinazofanyika kwa kiwango kikubwa vijijini ni kilimo na ufugaji, ambazo zinahitaji ardhi.

Kinamama ndiyo washiriki na wazalishaji wakubwa wa mazao na bidhaa zinazopatikana vijijini kwavile ndiyo washiriki kwa kiwango kikubwa wa kilimo, lakini wengi vijijini hawamiliki ardhi wala hajawezeshwa kumiliki rasilimali hiyo muhimu.

Hivyo serikali na wadau huu ndiyo wakati wa kuweka mkazo kwenye kuwapa wanawake hasa wa vijijini umiliki wa ardhi ili wawe na uhakika wa kufanya shughuli za kilimo kwa ufanisi na mafanikio.

Vilevile, wanawake wa vijijini wanapaswa kupewa kipaumbele katika mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ili wawe sehemu muhimu ya wanufaika wa mikakati hiyo.

Wanawake wa vijijini wanahitaji kuelimishwa kuhusu mikopo isiyo na riba inayotolewa na Halmashauri za Wilaya kwao, vijana na watu wanaoishi na ulemavu.

Aidha, wafahamishwe kuhusu fursa na uwezeshaji unaotoka kwenye serikali kuu katika kuwainua kiuchumi hii ni kwasababu si kinamama wote wa vijijini wanaojua uwepo wa fedha zinazotengwa kwa ajili yao hasa mikopo ya halmashauri.

> Taifa haliwezi kusonga mbele kimaendeleo kama wasichana na wanawake hawatapewa kipaumbele na fursa sawa katika sekta ya elimu na nyingine muhimu.

Kuwajumuisha wanawake kikamilifu katika shughuli za kiuchumi, kielimu na kisiasa kutaharakisha kasi ya maendeleo kuanzia kwenye kaya, jamii na taifa, kwavile wameonyesha uwezo mkubwa wa kuchapakazi hasa za kilimo, ufugaji, biashara na uwekezaji vijijini na hata mijini.

Serikali kwa upande wake, inalo jukumu la kuthamini kazi kubwa inayofanywa na wanawake kwa kuwawezesha kiuchumi ili kuwaondoa katika umaskini hasa wale wanaoishi vijijini.

Pia, taasisi za fedha kwa upande wake, ziwaelimishe kuhusu masuala ya fedha, uwekezaji, utunzaji mitaji na uendeshaji biashara lakini pia wapunguze masharti ili kuwapa fursa kinamama vijijini kunufaika na huduma za kibenki ili kujiinua kimaisha, uchumi, kisiasa na kimaendeleo.

Pamoja na uwepo wa mahitaji mengi ya wanawake, ni vyema suala la elimu na kuwezeshwa kiuchumi kwa hasa wanaoishi vijijini likapewa msukumo mkubwa kusaidia ustawi wa jamii na taifa kwa haraka.

Kasi kubwa ya maendeleo duniani kwa sasa inapaswa kumgusa kila mtu, hivyo hata kinamama wanaoishi vijijini hawapaswi kubaki nyuma katika nyanja za elimu, siasa, biashara na uchumi.

Kwa Tanzania wanawake ni zaidi ya nusu ya raia wote, hivyo ni kundi kubwa ambalo mafanikio yake yanageuza taswira ya maendeleo ya jamii na ya nchi.

Kwahiyo, kulitenga na kulibagua kundi hili ni kurudisha nyuma jitihada za kimaendeleo kuanzia siasa na uchumi.


Pia, juhudi za serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na wadau wengine kuboresha huduma za kijamii kama afya, maji, na nishati ya umeme zinawagusa moja kwa moja wanawake wa vijijini.

Upatikanaji wa huduma bora za kijamii kwa ukaribu, zitawaondolea kero za kutembea na kusafiri umbali mrefu kuzipata huduma hizo.

Mikakati ya kumwinua mwanamke wa kijijini iendelee kwa kasi kwavile kumwinua mwanamama ni kuinua nchi na kila mmoja kwakuwa ili kufanikisha maendeleo kinamama wanahusika kila upande.

**Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali Dodoma.**
**Maoni: 0620-800462.**

# Wakuu mikoa, wilaya wasaa wa manispaa mpya ni sasa



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Katibu Mtendaji wa Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Mitaji ya Maendeleo (UNSDF), Preeti Sinha, Ikulu Jijini Dar es Salaam. **PICHA: IKULU**

**Na Mwandishi Maalumu**

NDUGU zangu kuna vitu kwa macho ya kawaida huwa havionekani, lakini kwa utulivu wa hekima chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, vinaweza kukamilika kwa wakati na kuonekana bayana.

Rais Samia Suluhu hivi karibuni amekutana na kuzungumza na Katibu Mtendaji wa Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Mitaji ya Maendeleo (UNCDF), Preeti Sinha.

Katika mazungumzo hayo Rais na Preeti wanagusia namna ya kuzijengea uwezo kifedha serikali za mitaa kwa kuzitafutia njia mbadala za kujiendesha zenyewe bila kutegemea serikali kuu kwa kuanzisha miradi ya maendeleo.

Wanachotaka viongozi hao ni kuona manispaa zinawekeza kupitia Municipal Investment Financing, mradi utakaoweza kusaidia upatikanaji wa fedha kwa serikali za mitaa kupitia uanzishwaji wa hati fungani. (Municipal Bonds)

Municipal Bonds zitafanyaje kazi gani? Hili ni swali gumu ambalo wengi tuajiuliza wanahisa watakuwa ni kinanani..?

Ni kweli jambo hili kwetu ni jipya na mtihani upo kwa wakurugenzi, wakuu wa mikoa na wilaya katika halmashauri mbalimbali nchini kutegua kitendawili hicho.

Hati fungani za manispaa zitakuwa chini ya manispaa na kuratibiwa na manispaa ya eneo linahusika. Utaratibu huu utaziwezesha halmashauri kutafuta vyanzo vya pesa za kusaidia kukamilisha miradi yao ya maendeleo na hapa wanahisa wa Municipal Bonds au hati fungani za manispaa watafaidika kupata gawio kupitia kwenye miradi watakayoibuni na kuwekeza.

> Kwa upande mwingine ni mtihani mwingine mkubwa kwa wateule wa Rais Samia kusimamia maendeleo yenye kushikika na kuonekana kwa macho ya kibinadamu si kuishia kwenye makaratasi pekee.

Kaa la moto kwa Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Hoja hii haiwezi kupingwa na yeyote yule katika awamu hii ya sita Rais Samia ni mpole na mnyenyekevu thabiti kwenye misimamo na dhamira ya kweli kuwavusha Watanzania. Huko ndiko anapotaka kuwapeleka kwenye maendeleo endelevu.

Upole wa Rais Samia usiwe kigezo cha Wizara ya TAMISEMI kushindwa kuwavusha wananchi walioko kwenye halmashauri mbalimbali nchini kwenye mkakati huu wa kila halmashauri kuwezeshwa na kujiwezesha kujitegemea pasipo kuiegemea serikali kuu.

Kwa upande mwingine ni mtihani mwingine mkubwa kwa wateule wa Rais Samia kusimamia maendeleo yenye kushikika na kuonekana kwa macho ya kibinadamu si kuishia kwenye makaratasi pekee.

Mfano ujenzi wa miundombinu kama barabara, madaraja makubwa , miradi ya kijamii kama hospitali na shule.

Wanachotakiwa kufanya viongozi wa halmashauri ni kutoa municipal bonds au hati fungani za manispaa , hizi ni kama treasury bonds zinazotolewa na serikali kuu ila sasa hizi zitatolewa na manispaa zinazohusika.

Manispaa zitawalipa bond holders kupitia vyanzo vyao mbalimbali vya mapato vilivyopo katika miradi ya kimaendeleo iliyoanzishwa.

Kwa kuwa jambo hili ni geni ni wazi wananchi wanategemea kuona mpango kazi kutoka kwa watendaji husika wakiwaeleza kwa kina jambo hilo la Rais Samia linatekelezwa kwa ukubwa gani...?

> Ni jukumu la manispaa husika kuhakikisha jambo hili linafanyika kwa nia moja. Kwa mfano ukizungumzia 'Tiger Economies' hii ndiyo njia ya kukuza uchumi kwa kasi.

Moja ya faida kubwa katika mpango huo ni serikali kuu kupunguziwa mzigo wa kuzihudumia serikali za mitaa.

Lingine ni kuwa manispaa ikishindwa au kukiuka masharti ya kulipa bond itabidi wakamate mali za manispaa husika ili kufidia deni lao.

Mfano, pale ambapo huduma zilitakiwa kuwa bure itabidi ziwekwe chini ya usimamizi wa bond holders, ili watu walipie huduma ili kufidia deni. Kama Shirika la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) linavyofanya kwenye daraja la Kigamboni.

Ni jukumu la manispaa husika kuhakikisha jambo hili linafanyika kwa nia moja . Kwan mfano ukizungumzia 'Tiger Economies' hizi ndiyo njia ya kukuza uchumi kwa kasi.

'Tiger economy' ni hoja zinazorejea uchumi unaokua kwa kasi katika mataifa ya Asia Kusini Mashariki mfano Korea Kusini, Taiwani Singapore na Hong Kong.

Rais Samia nia yake ni kuwaletea Watanzania maendeleo hivyo, sitashangaa kuona 'tumbutumbua' nyingi kwa wakati huu. Aidha, sitashangaa kuona kasi ya maendeleo Mkoa wa Simiyu inaizidi ya Arusha au Kigoma ikipita kwa kasi Dodoma.

Maana manispaa ambazo usimamizi wake wa fedha si mzuri, bond zake zinaweza kukosa soko.

Ni wakati sahihi kutimiza ile kauli mbiu ya kazi iendelee kwa kujua kwamba nafasi walizopatiwa wakuu wa mikoa, Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya ni huduma kwa wananchi.

Rais Samia si muumini wa mapambio na unyang'anyi, ni muumini wa akili haya tuonyesheni uwezo wenu.



## Vijana wapewa mchongo fursa ukuaji teknolojia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

VIJANA nchini wametakiwa kutumia fursa ya ukuaji wa teknolojia duniani kubuni vitu vitakavyowawezesha kujiajiri ili kukabiliana na tishio la mashine kuchukua ajira zinazofanywa na binadamu.

Mkurugenzi mkazi wa shirika lisilo la kiserikali la Girl Effect, Dolorosa Duncan, alibainisha hayo juzi kwenye mjadala kuhusu mchango wa vijana katika maendeleo ya nchi ulioandaliwa na Asasi za kiraia ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Azaki.

Duncan alisema vijana wanatakiwa kutumia fursa ya ukuaji wa teknolojia duniani kubuni vitu mbalimbali vya kujipatia ajira ili kukabiliana na changamoto hiyo.

"Ukuaji wa teknolojia una changamoto zake pia una fursa ambazo sisi kama vijana tukizitumia vizuri tunaweza kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira duniani," alisema Duncan.

Pia alisema hivi sasa duniani kuna tishio la baadhi ya ajira kuchukuliwa na mashine kutokana na ukuaji wa teknolojia, hivyo vijana hawana budi kujiandaa na changamoto hiyo.

Kadhalika, alisema kupitia teknolojia zipo fursa nyingi za ajira ambazo vijana kama watazitumia vizuri zinaweza kuwatoa kimaisha na kuacha kuendelea kulalamika.

Alitoa wito kwa viongozi mbalimbali katika sekta binafsi pamoja na serikalini kuwaamini vijana na kuwapa nafasi ili wajifunze.

"Tunatakiwa kuwaamini vijana hata vijana waliofanikiwa kuna watu ambao waliwaamini wakawaacha wakose lakini leo hii wamekuwa viongozi wazuri katika nafasi mbalimbali", alisisitiza

Mkurugenzi Mtendaji wa The Foundation for Civil Society, Francis Kiwanga, alisema siri kubwa ya vijana kukuwa ni kufanya kazi zao vizuri.

"Kijana fanya kazi yako vizuri watu wataona tuu hii ndiyo siri kubwa ya kupata mafanikio hata kama uko wapi lakini kazi yako nzuri itakutambulisha lakini pia niwaambie kama unafanya kitu fanya usiogepe kwani neno hili limeandikwa kwenye biblia zaidi ya mara 365, hivyo vijana tusiogope," alisema.

# Asilimia 50 ya watoto mitaani matokeo ya ndoa zilizovunjika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASILIMIA 50 ya watoto wanaoishi mtaani wanatokana na ndoa zilizovunjika, imebainika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu(LHRC), Anna Henga, aliyasema hayo jana kwenye mjadala kuhusu namna asasi za kiraia zinavyochangia kwenye maendeleo ya taifa, katika kwenye wiki ya AZAKI inayoendelea jijini hapa.

Alisema ndoa nyingi zinavunjika kwa sasa na zinazalisha watoto wengi wanaoishi mitaani.

"Asilimia 50 ya watoto wanaoishi mtaani wanatokana na ndoa zilizovunjika. Tuligundua hili kutokana na kutoa msaada wa kisheria, tukawafuata watu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto tukawaambia jamani tunatakiwa kufanya kitu.

"Wakatushauri kuyafundisha mabaraza ya ndoa ili zisivunjike basi hata kama zitavunjika zisiwe nyingi na tusizalishe watoto wengi wanaokaa mtaani. Kwa hiyo tukafanya hivyo, tukakubaliana tutengeneze sera ya mabaraza ya ndoa na sasa iko kwenye hatua za mwisho,"alisema.

Alibainisha kuwa wiki iliyopita walikuwa mkoani Morogoro kwa ajili ya mapitio ya sera hiyo kwa kushirikiana na wizara.

"Hapo inayoshughulika hivyo ni azaki moja, lakini ziko ngapi. Wengi tunafanya kazi nzuri sana kila mmoja akiamua kutoa ushuhuda wake wa kitu alichochangia nadhani tutakaa wiki nzima tunasikiliza shuhuda nzuri. Kwenye utawala wa sheria, asasi zina kazi kubwa lakini tujitahidi kuzitangaza zionekane,"alisema.

Hata hivyo, alisema asasi zinafanya kazi kubwa ya sheria na kuziangalia kabla hazipalekwa bungeni.

"Sisi ambao tunajishughulisha na sheria hakuna muswada ambao unapelekwa bila kutushirikisha sisi wadau. Tunaangalia, tunachambua hata Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ilivyokuja. Tuliangalia na kuchambua ilikuwa na changamoto nyingi kuliko zilizopo hivi sasa," alisema.

Alisema LHRC na Twaweza walifanya kazi hiyo ya kuchambua na asilimia 33 ya mapendekezo ya Azaki yalichukuliwa kwenye sheria hiyo.

"Pale mnapoona uzuri wa sheria kuna asilimia 33 ya mapendekezo ya Azaki, tumekuwa tukipitia miswada na inapokwenda bungeni inakuwa na maoni ya wadau na mengi wanachukua na sasa kuna miswada tunaendelea kuipitia tunaamini watachukua mapendekezo yetu kwasababu hata utashi wa kisiasa tunauona kwenye masuala ya utawala wa sheria,"alisema.

Kadhalika, alisema utafiti mbalimbali ambao hutolewa na asasi hutumiwa na watoa uamuzi.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (wa tatu kulia), akipata maelezo kutoka kwa Ofisa Ardhi Mteule wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Pirmin Mzenga, alipofanya ziara ya kushtukiza katika ofisi za ardhi za jijini humo jana. Kushoto ni Kamishna wa Ardhi nchini, Nathaniel Nhonge. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Ataka wenye magonjwa sugu, wajawazito kuchanjwa corona

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Waze na Watoto, Prof.Abel Makubi, amewashauri watu wenye magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu na wajawazito kupata chanjo ya corona aina ya Sinopharm ambayo inatolewa hivi sasa kwa kuwa haina madhara yeyote.

Pia ameshauri mtu asinywe pombe saa nne hadi nane kabla ya kupata chanjo ili kutochanganya pombe na dawa kwa kuwa haitazalisha kinga kwa ufanisi.

Prof. Makubi aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye mkutano wa kimkakati kati ya wizara hiyo, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na mashirika yasiyo ya kiserikali kujadili namna ya kupambana na corona kwa pamoja.

Alisema katika utoaji wa chanjo hushauriwa mtu anayeumwa akiwa amezidiwa sana asipewe chanjo hadi apate nguvu.

"Pia kama mtu ana 'allergy' (mzio) na chanjo, hatushauri achanje lakini kama mtu ana afya njema ana magonjwa haya mengine ambayo tunayajua kama sukari, presha, figo na kansa, unaenda kuchanja bila tatizo lolote,"alisema.

Alisema hakuna mazuio yoyote ya kumfanya mwananchi kwenda kuchanja.

Kadhalika, alisema kwa mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO), kama mtu amechanja chanjo aina ya JJ, hairuhusiwi kuchanja tena Sinopharm ambayo imeanza kutolewa hivi sasa.

"Mwongozo tulio nao WHO na serikali kwa sasa hivi ukichanja JJ au Jenssen huruhusiwi kuchanja tena hii Sinopharm. Naomba wananchi wasiwe na kutangatanga au wakashawishiwa na watu kuchanja na hii kwa kuwa ukichanja tayari umepata kinga. Huna haja ya kuunganisha zote mbili kwa kuwa sayansi haijaonyesha faida ya kuchanja JJ halafu ukachanja na Sinopharm," alisema.

Kuhusu ushirikiano na mashirika hayo, Katibu Mkuu huyo alisema waliahidi wako tayari kushiriki katika mapambano ya corona na kinachotakiwa kwa sasa ni kuhamasisha uchanjaji ambapo kwasasa kiwango kilichofikiwa cha kuchanja wananchi 50,000 kwa siku kabla ya JJ haijaisha.

"JJ ilishaisha kwasasa tunaendelea kuchanja kwa kutumia Sinopharm ambayo mtu anatakiwa kuchanja mara mbili tofauti na JJ, sasa tunawataka wananchi waitikie kurudi kupata chanjo ya pili ya Sinopharm, kwa kuwa inahitaji kuchanja mara mbili, na tumuona kazi hii serikali pekee haiwezi tumeona tushirikishe na wadau wengine kama mashirika haya na viongozi wa dini,"alisema.





# Waiangukia serikali matengenezo mashine

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKULIMA wa mpunga katika skimu ya umwagiliaji ya Mbuyuni katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, wameomba serikali na wadau wa kilimo kuwasaidia kuboresha mashine za kuvunia mpunga ili kuepusha upotevu wa mazao unaotokana na kuchelewa uvunaji.

Walitoa ombi hilo wakati wa ziara ya kukagua miradi ya kilimo na mifugo iliyofanywa na maofisa wa taasisi isiyo ya kiserikali inayohusika na mambo ya kilimo ya Agricultural Non-State Actors Forum (ANSAF) na maofisa wa Mtandao wa Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali Mkoa wa Mbeya (MBENGONET).

Mwenyekiti wa Skimu hiyo, Fashon Madege, alisema mwaka 2015 serikali iliwapatia mashine 11 za kuvunia mpunga lakini mpaka sasa wamebaki na mashine tatu pekee zinazofanya kazi hali ambayo imepunguza ufanisi katika uvunaji.

Alisema kati ya mashine hizo 11, halmashauri ilizichukua tatu na hawajui zilipelekwa wapi, mbili zilishindwa kufanya kazi kutokana na teknolojia ya matengenezo yake kushindwa kuendana na mazingira na tatu zimekufa.

Madege alisema kati ya mashine hizo tatu zilizokufa ni moja pekee ndiyo inayotengenezeka lakini bado wameshindwa kuitengeneza kutokana na kutokuwa na uwezo wa kiuchumi.

"Tunaomba kama inawezekana serikali itusaidie kununua mashine za kuvunia za kisasa, kwa sasa zimekuja mashine ambazo ni za kisasa na zinasababisha za kwetu kukosa soko, kwa sasa tunaomba Serikali itusaidie kuboresha mashine hizi," alisema Mdege.

Pia aliomba serikali iwasaidie kuboresha mashine yao ya kukoboa mpunga akidai kuwa uendeshaji wake ni mgumu kutokana na kutumia umeme mwingi tofauti na mashine zingine.

Katibu wa Kamati ya Ufuatiliaji wa Miradi wa MBENGONET Wilaya ya Mbarali, Elisha Mwanikawaga, alisema ufuatiliaji wa miradi wa kamati hiyo ulibaini kuwa kutelekezwa kwa mashine hizo kunaisababishia serikali harsara kubwa.

Alisema kwa mazingira ya Wilaya ya Mbarali yalivyo yanatakiwa mashine aina ya Kubota ambazo ndizo zinavumilia suluba lakini zingine hazina uwezo wa kuhimili.

Alisema pamoja na mashine hizo pia serikali inatakiwa kuwasaidia wananchi kuboresha skimu yao ya umwagiliaji kwa kusakafia mfereji ili kuepusha upotevu wa maji kabla hayajafika mashambani.

"Kitu kingine tulichokibaini ni kwamba wananchi hawa walikabidhiwa mashine hizi bila maandishi yoyote na hata zile mbili zilizochukuliwa hazikuchukuliwa kwa maandishi, hivyo tunaomba utaratibu huu uboreshwe," alisema Mwanikawaga.

Mratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali wa Wilaya ya Mbarali (USANGONET), Tedy Mhagama, alisema skimu nyingi za wilaya hiyo zinakabiliwa na matatizo mengi ambayo walibaini yanakwamisha maendeleo ya skimu na vyama vya ushirika.




Mwenyekiti wa Jukwaa la Wanawake wanaoishi na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI Tanzania, Joceline Mtono (kulia) na Meneja wa Baraza la Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI Tanzania (NACOPHA) Kanda ya Mbeya, Ferdinand Mazuni (wa pili kulia), wakikabidhi vifaa vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona kwa viongozi wa Konga ya Jiji la Mbeya pamoja na maofisa wa Jiji la Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## NACOPHA yawasaidia vifaa wanaoishi na VVU Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BARAZA la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (NACOPHA), kupitia mradi wake wa 'Hebu Tuyajenge' chini ya ufadhili wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani, limetoa vifaa mbalimbali vya kujikinga na maambukizi ya corona kwa wanachama wake wa Mkoa wa Mbeya.

Aidha, baraza hilo limewahamasisha wanachama wake kupata chanjo ya kujikinga na corona ambayo inatolewa bure na serikali huku likiwataka kuchukua tahadhari mbalimbali zinazoshauriwa na wataalamu wa afya kujikinga na ugonjwa huo. Vifaa vya kujikinga na corona vilivyotolewa na baraza hilo kwa wanachama ni ndoo za maji tiririka, sabuni za kunawia mikono, vitakasa mikono na barakoa.

Akikabidhi vifaa hivyo juzi katika ofisi za konga ya Jiji la Mbeya, Meneja wa NACOPHA Kanda ya Mbeya, Ferdinand Mazuni, alisema vifaa hivyo vimetolewa na baraza hilo katika halmashauri zote nchini ambazo zinatekeleza mradi wa 'Hebu Tuyajenge'.

Alisema kwa Mkoa wa Mbeya, mradi huo unatekelezwa katika halmashauri za ya Jiji la Mbeya na Rungwe na kwamba vifaa hivyo ni muhimu katika kukabiliana na janga la corona.

"Sisi kama baraza tunapiga vita dhidi ya corona tangu ugonjwa huu ulipoanza. Tulianza kutoa elimu kwa watu wetu na hata kutoa vifaa vya kujikinga lakini kwa sasa baada ya mfadhili wetu kutusaidia, tumeona ni vyema tugawe vifaa hivi kwa wenzetu," alisema Mazuni.

Mwenyekiti wa Konga ya Jiji la Mbeya, Deogratius Kisunga, alisema vifaa vilivyotolewa vitawanufaisha zaidi ya watu 3,000 wa jiji hilo wanaoishi na VVU na kwamba vitagawiwa kwenye vikundi vilivyoko katika kila kata.

Aliushukuru uongozi wa baraza hilo Taifa kwa kutoa vifaa hivyo akieleza kuwa vitawasaidia kujikinga na virusi hivyo huku akiwataka wanufaika kuhakikisha wanavitumia ipasavyo.

Pia aliwataka wanachama wote kuepuka opotoshaji unaoenezwa na baadhi ya watu kuhusu chanjo ya Corona kwa madai kuwa watu hao wana nia ovu ya kurudisha nyuma juhudi za serikali kwenye vita dhidi ya ugonjwa huo.

"Kinachosikitisha ni kwamba wanaosema vibaya kuhusu chanjo ni wale ambao hawajachanja, waliochanja wanasema chanjo haina madhara sasa ninachowashauri ni kwamba tuwasikilize wataalamu wa afya badala ya kuwasikiliza wapotoshaji hawa," alisema Kisunga.

## Wapewa elimu ya kilimo bora

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

WANANCHI wa kata sita za Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, wamepatiwa elimu ya kilimo bora kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa chakula ili kuepuka kukumbwa na tatizo la njaa ambalo limekuwa likiwakabili kila mwaka.

Aidha, wananchi hao wamepatiwa elimu ya uhifadhi wa chakula ili kuepuka upotevu wa mazao yao baada ya kuvuna unaotokana na kuoza ama kuliwa na wadudu.

Elimu hiyo ilitolewa mwishoni mwa juzi na Shirika la Maendeleo la ADP Mbozi kwa kuanzisha programu hiyo ya kutoa elimu kwa wakulima wa eneo hilo ili kuwanusuru na tatizo la njaa ambalo linadaiwa kuwa limekuwa tatizo sugu.

Mkurugenzi wa ADP Mbozi, Daria Rugumira, alisema wakulima wa eneo hilo wamekuwa wakizalisha chakula kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na mahitaji yao hali ambayo ndiyo ilikuwa inakuwa chanzo cha njaa.

Aidha, alisema wananchi hao wamekuwa wakiuza sehemu kubwa ya mazao yao ili kupata fedha za kujikimu na hivyo kubaki na kiasi kidogo cha chakula.

"Tunataka kuwasaidia wakulima hawa ili waongeze uzalishaji na wawe na uwezo mkubwa wa kutunza chakula kwa ajili ya matumizi, tumeshalibaini tatizo lao na ndio maana tumeamua kuwasaidia elimu ya kukabiliana na tatizo hili," alisema Rugumira.

Baadhi ya wananchi waliopatiwa elimu hiyo kuanzia uzalishaji shambani hadi kuhifadhi chakula majumbani walisema elimu hiyo itawanufaisha kwa kiasi kikubwa wakidai kuwa walifundishwa vitu vingi vinavyohusiana na kilimo.

Mmoja wa wananchi hao, Anna Nzuwa, alisema kwa muda mrefu walikuwa wanakumbwa na njaa kutokana na uzalishaji kuwa mdogo na kuhifadhi chakula kwa kutumia njia ambazo zilikuwa zinasababisha chakula kuharibika.

Alisema baada ya kupata elimu hiyo sasa wataondokana na tatizo la njaa na watakuwa na uhakika wa kuhifadhi chakula cha kutumia mwaka mzima.

"Hizi mbinu za kutunza chakula ni nzuri sana kwetu na nina uhakika zitakuwa suluhisho, tulikuwa tunabaki bila akiba kwa sababu uzalishaji ulikuwa chini na tulikuwa tunauza sana," alisema Nzuwa.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songwe, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Galula, John Ntakoma, alisema serikali ya wilaya hiyo itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuboresha uzalishaji wa mazao mbalimbali.

Alilishukuru shirika hilo kwa kazi ambayo linafanya ya kuelimisha wananchi akidai kuwa elimu wanayopata itawasaidia wananchi kuongeza uzalishaji.



# Hemed ataka ufumbuzi uharibifu mazingira

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

VIONGOZI wa serikali mikoa na wilaya, wametakiwa kushirikiana na shehia kupata ufumbuzi wa changamoto ya uharibifu wa mazingira katika eneo la Mpiga Duri Maruhubi, Zanzibar.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alieleza hayo jana alipofanya ziara maalum ya kukagua eneo la Mpiga Duri lililoathiriwa kwa shughuli za ukataji wa mikoko na uchimbaji wa mchanga.

Alileza kuwa, kuna haja ya kutoa taaluma kwa wananchi waliolizunguka eneo hilo, ili kuwajengea uelewa juu ya dhana ya uharibifu wa mazingira pamoja na athari zake kwa jamii.

Alisema tatizo la uharibifu wa mazingira katika eneo hilo ni kubwa, jambo litakalosababisha athari kwa maji ya bahari kuvamia katika makazi ya watu, kutokana na ukataji ovyo wa misitu aina ya mikoko, sambamba na harakati za uchimbaji wa mchanga.

Hemed alisema serikali haipendi kuona mivutano kati ya wananchi wake, hivyo aliwaagiza viongozi wa serikali ya Mkoa wa Mjini Maghabari Unguja na shehia kuangalia namna bora ya kuipatia ufumbuzi changamoto hiyo kwa kuwafikishia taaluma wahusika wa vitendo vya uharibifu wa mazingira.

Aidha, alisema serikali haitasita kumchukulia hatua mtu yeyote atakayebainika kushiriki katika vitendo vya uharibifu wa mazingira, huku akiwaasa wananchi kuachana na vitendo hivyo.

Naye, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya, alisema jiografia ya eneo hilo ni la maficho na linapelekea kutumiwa na wahalifu kufanya vitendo viovu ikiwmo vya madawa ya kulevya.

Alisema katika kuhakikisha vitendo vya uharibifu wa mazingira na vitendo vya uhalifu vinatokomezwa katika eneo hilo, hakuna budi kupatikana kwa msaada kutoka kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuidhibiti kadhia hiyo. Sheha wa Shehia ya Muembe Makumbi, Halima Azan Makame, alisema, eneo la Mpiga Duri linakabiliwa na kadhia ya uharibifu wa mazingira kwa muda mrefu sasa, inayosababishwa na wahalifu kutumia zana za jadi kwa kuwashambulia viongozi wa shehia wanaofanya doria katika eneo hilo.

Kufuatia changamoto hiyo, Sheha Halima alitoa rai kuwekwa kwa kituo maalum kitakachosaidia kuendesha doria kwa muda wote.

## Jaji Makungu ajivunia kasi usikilizaji kesi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAJI wa ,mahakama ya rufaa nchini, Omar Othman Makungu, amesema kesi za udhalilishaji wa kijinsia ni miongoni mwa vipaumbele vya mahakama, kutokana na kuwapo malalamiko mengi na wingi wa kesi hizo, ambazo baadhi yake zilikwama kwa sababu mbalimbali.

Aliyasema hayo jana wakati akimkabidhi Ofisi ya Mahakama Kuu Zanzibar Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdalla, aliyeapishwa hivi karibuni kushika wadhifa huo na Rais wa Zanzibar, Dk.Hussein Ali Mwinyi.

Makungu ambae alikuwa Jaji Mkuu wa Zanzibar, alisema uongozi wa mahakama ulichukua juhudi za kuhakikisha kesi hizo zinasikilizwa kwa kasi na kupewa kipaumbele kwa kuzishirikisha baadhi ya taasisi zinazofanya upelelezi, ikiwamo Jeshi la Polisi na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Alisema katika kipindi cha miezi sita matokeo yake yameonekana, ikiwamo kesi hizo kutolewa hukumu, hatua ambayo kwa kiasi kikubwa jamii imerudisha imani kwa mahakama, ambazo zimekabidhiwa majukumu ya kutoa haki.

"Miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika mahakama zetu ni kusikiliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia kwa kasi ya aina yake na kuzitolea hukumu hatua ambayo jamii imejenga matumaini kwa vyombo hivyo,"alisema.

Aidha, Jaji Makungu alimtaka Kaimu Jaji Mkuu kulipatia ufumbuzi tatizo la uhaba wa fedha pamoja na rasilimali watu, ikiwamo mahakimu ambao ndio wanaofanya kazi ya kusikiliza kesi na kutoa hukumu. Kaimu Jaji Mkuu Ramadhan aliwaomba watendaji kumpa kila aina ya ushirikiano, ili kufanikiwa katika utekelezaji wa majukumu makubwa ya kusimamia haki na sheria.

Alisema amejipanga kuhakikisha changamoto mbalimbali zinazoikabili mahakama kuu zinapatiwa ufumbuzi, huku akiwataka majaji na mahakimu kuongeza kasi ya kusikiliza kesi kwa wakati.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abadulla (mwenye suti ya kijivu), akitembelea eneo la Mpigaduri, Maruhubi Wilaya ya Mjini, Unguja jana, kukagua eneo lililoharibiwa kutokana na ukataji wa mikoko na uchimbaji wa mchanga. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mwinyi awataka mabalozi kutangaza fursa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekutana na kufanya mazungumzo na mabalozi wanaokwenda kuiwakilisha Tanzania nje ya nchi na kusisitiza haja ya kwenda kuzitangaza fursa za kujenga uchumi.

Pamoja na mambo mengine, amewataka kuitangaza sera ya uchumi wa buluu, ambayo ndio dira ya uchumi wa Zanzibar.

Mabalozi ambao alikutana nao juzi Ikulu Zanzibar ni Balozi Anisa Mbega anayekwenda kuiwakilisha Tanzania nchini India, Balozi Togolani Edriss Mavura anayekwenda kuiwakilisha Tanzania nchini Korea Kusini, Balozi Innocent Shiyo anayekwenda kuiwakilisha Tanzania nchini Ethiopia.

Katika mazungumzo hayo, Rais Dk. Mwinyi aliwaeleza Mabalozi hao, kwamba nchi kama Korea Kusini imepiga hatua kubwa katika kuitumia bahari kama sehemu mojawapo ya kuimarisha uchumi wake ikiwamo na kuwa na viwanda vingi vya uvuvi, bandari na viwanda vya meli, hatua ambayo inaweza kusaidia katika kuendeleza Sera ya Uchumi wa Buluu kwa Zanzibar.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi aliwataka mabalozi hao kwenda kuitangaza Zanzibar kiutalii kutokana na vivutio vyake kadhaa vilivyopo hasa kwa nchi za Korea Kusini na India ambako bado watalii wanaoitembelea Zanzibar sio wengi.

Rais Dk. Mwinyi aliwaeleza mabalozi hao juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukuza uchumi wake kupitia ujenzi wa bandari ya kisasa, ambayo itajumuisha shughuli mbalimbali ambapo pia, itahitaji wawekezaji.

Alisema mikakati iliyowekwa katika kuhakikisha inaijengea uwezo Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) iweze kufanya kazi ipasavyo na kuwa kituo maalum kitakachotoa huduma zote za uwekezaji kwa muda mfupi.

Pia aliwataka Mabalozi hao kusaidia kutafuta soko kwa ajili ya zao la mwani, kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wa zao hilo sambamba na kutafuta wawekezaji, kwa ajili ya kuja kuekeza katika sekta ya viwanda pamoja na gesi asilia Zanzibar.

Mabalozi hao walimhakikishia Rais Dk. Mwinyi kuwa juhudi za makusudi watazichukua katika kuhakikisha wanatekeleza vyema majukumu waliyopewa na kutumia fursa hiyo kutoa shukurani zao kwa Rais kutokana na maelekezo aliyowapa.

## HABARI KITAIFA

## Aliyesumbuliwa mtindio miaka 15 afariki

**Na Devota Mwachang'a**

MTOTO Neema John aliyesumbuliwa na tatizo la mtindio wa ubongo (CP) kwa miaka 15, amefariki dunia nyumbani kwao Mtaa wa Machimbo Lumo wilayani Temeke, Dar es Salaam.

Lydia Selestine, mama wa mtoto huyo akizungumza baada ya maziko yaliyofanyika mwishoni mwa wiki, aliishukuru Nipashe kwa kuchapisha taarifa kuhusu tatizo la mtoto wake na kuwezesha kupata msaada toka kwa wasamaria wema.

Nipashe kupitia toleo laka Na. 0580726 la Alhamisi Oktoba 07, mwaka huu, ilichapisha makala iliyoangazia kwa kina matatizo yaliyomkabili mtoto huyo tangu akiwa na umri wa miezi miwili.

"Ninawashukuru sana Nipashe kwa kuandika taarifa za mtoto wangu, watu waliojitokeza kutupatia msaada. Baadhi walisema wamesoma habari na kuona picha ya Neema kwenye gazeti, Mungu awabariki," alisifu mama huyo aliyezungumza kwa simanzi.

Aliendelea: "Nilimzoea mwanangu bila kujali hali yake ya ulemavu, alikuwa faraja yangu, rafiki niliyekuwa naye muda wote nikimsemesha bila kujali kuwa hakuwa na uwezo wa kuongea wala kutoa ishara."

Mmoja wa waombolezaji, Joseph Mbigiri, alisema: "Kwa kiasi kikubwa kuchapishwa kwa taarifa za marehemu Neema kwenye gazeti kuliwafanya watu kujitojeza kumsaidia kifedha na wapo waliotaka kumsaidia zaidi ila Mungu amemchukua, hatuna la kusema zaidi ya kuombea pumziko la amani."

Neema alizaliwa Novemba 15, 2006 akiwa na uzito mkubwa kilogramu 6.8. Katika umri wa miezi miwili tu, aliugua homa kali iliyosababisha apate tatizo la CP, hivyo kutokuwa na uwezo wa kusongesha mwili wake kwa namna yoyote.



Mratibu wa Kanda wa Child Help International, Janeth Manoni, akizungumza katika kongamano la kujadili vikwazo vinavyowakumba watoto wenye ulemavu wa kichwa kikubwa na mgongo wazi, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Daktari Bingwa wa Mishipa na Fahamu kutoka Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Dk. Hamis Shabani, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wazazi wa Watoto Wenye Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi (ASBAHT), Abdul-hakimu Bayakub na Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Dar es Salaam, Judith Kimaro. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwenyekiti aongoza mbio kumrithi Nasha

**Na Cynthia Mwilolezi,**

ARUSHA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, Emmanuel Ole Shangai, ameongoza kwenye mchakato wa kura za maoni kupitia CCM wa ubunge Jimbo la Ngorongoro/

Shangai amepata kura 420 kati ya 940 zilizopigwa kwa ajili ya kumrithi aliyekuwa mbunge wa Jimbo hilo, William Ole Nasha. Nasha, ambaye alikuwa Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Wazri Mkuu (Uwekezaji), alifariki dunia mwezi uliopita.

Akitangaza jana wilayani humo matokeo ya kura za maoni jana ambazo zilifanyika katika Uwanja vya Ndege Orkanda uliopo Mji Mdogo wa Wasso-Loliondo, Msimamizi wa uchaguzi ambaye ni Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Arusha, Gerald Munusi, alimtangaza Shangai kuongoza katika kura hizo kati ya kura 943 zilizopigwa, huku kura 3 zikiharibika.

Munisi alisema baada ya matokeo hayo, chama kitaendelea na mchakato mwingine na baadaye kitamleta mgombea sahihi.

Alisema aliyeshika nafasi ya pili ni Joseph Parsambei (187), Elias Ngorisa aliyeshika nafasi ya tatu (136) na nafasi ya nne ilishikwa na Sirael Nambololo (61).

Wengine ni Kokel Melubo (56), Moloiment Olemoko (21), Mesha Singolyo (19), Patrick Girigo (10) huku, Elizabeth Gibaseya na William Saning'o wakifungana kwa kura 7 kila mmoja.

Wengine ni Daud Olemtara (5), Elifuraha Laltaika (4), Rose Ngilo (3), Elinora Sangei (2), Elias Nagol pamoja na Leyan Sabore wakifungana kwa kupata kura (1) kila mmoja na James Taki (0).

Shangai aliishukuru CCM wilaya na mkoa, wagombea wenzake pamoja na wajumbe, kwa kazi kubwa waliofanya.

"Kwa sasa sina la kusema kwa sababu hizi ni kura za maoni na endepo chama kitaniamini na kunipa ridhaa basi hawatajuta kunipitisha," alisema.

# Mulamula: Ushirikiano na Marekani ni wa faida

**Na Romana Mallya**

SERIKALI ya Tanzania imekiri kuwa uhusiano mkubwa wa miaka 60 kati yake na Marekani umeleta matokeo makubwa na ya kihistoria katika maeneo mbalimbali ikiwamo sekta ya elimu.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akifungua mkutano maalum uliojulikana kama 'Pamoja 60 Conference'.

Mkutano huo ambao uliandaliwa kwa ushirikiano baina ya Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini (REPOA) na Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania, uliangazia mafanikio ya ushirikiano wa nchi hizo kwa miaka 60 iliyopita.

Balozi Mulamula akihutubia kwa njia ya mtandao kupitia video iliyorekodiwa, alisema dhamira ya Tanzania ni kuendelea kufanya kazi kwa karibu na Marekani na kuimarisha uhusiano baina ya nchi hizo ambao uliimarishwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na John Kennedy wa Marekani.

Alisema maadhimisho hayo ya miaka 60 yanashuhudia hatua nyingine muhimu katika urafiki huo wa kihistoria kwa pande zote mbili.

"Tangu Tanzania ipate uhuru mwaka 1961, Marekani imekuwa ikisaidia juhudi za Tanzania za maendeleo katika sekta ya elimu, afya, maji, kilimo, demokrasia na haki za binadamu, miundombinu na teknolojia.

Alisema katika kuhakikisha misaada inayotolewa na Marekani inaendelea kuwanufaisha Watanzania kwa sasa na baadaye, serikali inahakikisha inaimarisha demokrasia na haki za binadamu, mapambano dhidi ya rushwa na uhalifu wa kupangwa pamoja na kuimarisha amani na umoja.

Mkurugenzi Mtendaji wa REPOA, Dk. Donald Mmari, alisema ziko programu mbalimbali katika vyuo ambavyo vinashirikiana na vya Marekani katika kuvijengea uwezo katika utafiti katika sekta ya afya, uchumi na nyingine.

Alisema REPOA ni miongoni mwa taasisi ambazo zimenufaika na uhusiano kati ya nchi hizo mbili ambapo baadhi ya watafiti wake wamepata elimu nchini Marekani.

Balozi wa Marekani nchini Tanzania, Dk. Donald Wright, alisema kama ilivyo kwa miaka 60 iliyopita, Marekani inaendelea na dhamira yake ya kushirikiana na serikali ya Tanzania kuimarisha sekta ya elimu kote nchini.

Alisema kwa miaka mitano pekee, Marekani kupitia shirika lake la USAID limechangia zaidi ya Dola za Marekani milioni 65 kwenye mfumo wa elimu ya msingi.

Pia alisema wanaunga mkono mfumo wa elimu ya sekondari ili kuongeza ushiriki wa watoto wa kike kubaki shuleni.


**SIMBA CEMENT**
STRENGTH WITHIN

## CAUTIONARY NOTICE TO MEMBERS

**PROPOSED ACQUISITION BY SCANCEM INTERNATIONAL DA OF 68.33% OF THE SHARES IN TANGA FROM AFRISAM MAURITIUS INVESTMENT HOLDINGS LIMITED**

**TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY (DSE: TCPLC)**
**(Incorporated in the United Republic of Tanzania) ("Tanga" or "the Company")**

Shareholders are referred to the joint announcement made by HeidelbergCement AG ("Heidelberg Cement") and AfriSam Mauritius Investment Holdings Limited ("AfriSam") on the 26 October 2021 ("the HeidelbergCement Announcement"), where it was announced that Scancem International DA ("Scancem"), a subsidiary of HeidelbergCement, and AfriSam have finalised the terms upon which Scancem will acquire AfriSam's 68.33% shareholding in Tanga ("the Acquisition"). Shareholders are urged to read the joint announcement by AfriSam and HeidelbergCement.

The Tanga Board of Directors ("Board") was duly informed of the Acquisition by AfriSam shortly after the Acquisition transaction agreements were concluded. The Board will now take appropriate advice and follow the steps required of it in terms of the Capital Markets and Securities (Substantial Acquisitions, Takeovers and Mergers) Regulations, 2006. The Board will communicate further with the shareholders in due course in this regard.

The Acquisition is subject to the fulfillment, or if applicable, waiver of a number of conditions precedent ("the Conditions") by 30 June 2022 or such later date as the parties may agree in writing. These Conditions are set out in detail in the joint announcement by AfriSam and HeidelbergCement. The indicative price per share to be paid by Scancem to AfriSam is TZS 3,157 per Tanga share ("the Acquisition Price"). The Acquisition Price is also subject to potential adjustments relating to debt, working capital and other expenses. HeidelbergCement and AfriSam cautioned that material uncertainty exists on the final Acquisition Price.

If the Acquisition becomes unconditional and is implemented, Scancem will acquire control of the Company. If this occurs, Scancem will, after the final Acquisition Price is determined, make a general offer to acquire the remaining shares in Tanga ("the General Offer").

Shareholders are cautioned that there is no certainty that all the Conditions to the Acquisition will be fulfilled, or waived, timeously. Therefore there is no certainty that the General Offer will be made. There is also material uncertainty on the final Acquisition Price.

The Company is also still trading under the cautionary announcement made on the 31 August 2021. Shareholders are accordingly advised to continue to exercise caution when dealing in Tanga's securities.

Further announcements will be made in due course.

**On behalf of the Board.**

**Lawrence Masha**
Chairman of the Board
27 October 2021

# NYOTA SIMBA SC WAIPONDA IKIIVAA POLISI TANZANIA LEO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikishuka dimbani leo kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Polisi Tanzania, huku ikiwa inaugulia kipigo cha mabao 3-1 ilichokipata Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana, wadau na wachezaji wa zamani wa timu hiyo wamezidi kuikosoa timu hiyo kutokana na namna walivyoruhusu mabao hayo wakieleza hayana tofauti na yanayofungwa katika mechi za bonanza.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba leo watashuka tena kwenye uwanja huo huo kucheza dhidi ya Polisi Tanzania, saa moja usiku.

Simba inaingia leo uwanjani huku wanachama na mashabiki wa klabu hiyo wakionekana kuchanganyikiwa juu ya mwenendo wa timu yao, lakini wakijawa na wasiwasi na viwango vya baadhi ya wachezaji wao na kauli za viongozi wao kuwa kuna wasaliti ndani yao.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu, mbali na kuwaomba radhi wanachama na mashabiki wa timu hiyo, pia amesema uongozi unafanya tathmini ya kina kuona nini kilitokea, hivyo kuwataka kuendelee kuiunga mkono kwenye mechi zinazoendelea za Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho Afrika.

"Kwanza kabisa nitoe pole kwa wanachama na mashabiki wa Simba nchini na duniani kote, si jambo ambalo lilitarajiwa. Timu ilicheza vema ugenini na hata kipindi cha kwanza, lakini kilichotokea kila mtu anajua. Uongozi unafanya tathmini kuona nini kilitokea na kuhakikisha hakitokei tena kitu kama hicho, tumeshuka kwenye shirikisho, tunaamini kuwa tutafanya vizuri, waendelee kuiunga mkono kwenye mechi hizo na za Ligi Kuu ambayo inaendelea ili kutetea ubingwa wetu," alisema mwenyekiti huo.

Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, amesema kuwa pamoja na kwamba Simba imepoteza, lakini hawaingii kwa kuwadharau, kwani ni timu nzuri na itakuwa ni kujidanganya kudhani kuwa msimu huu hawapo vizuri.

"Simba ni timu kubwa na nzuri, tusijidanganye. Ina kocha mzuri na wachezaji wazuri kwa hiyo itakuwa ni mechi ngumu. Nia siyo kuifunga Simba, nia yetu ni kupambana, tukipata pointi tatu sawa, ukiangalia hata mechi ya Ligi ya Mabingwa ambayo wametolewa, haikucheza vibaya, ila ilifungwa kutokana na makosa yao binafsi tu," alisema kocha huyo.

Polisi Tanzania ndiyo inayoongoza ligi mpaka sasa ikishinda mechi zote tatu, hivyo kuwa na pointi tisa, Simba ikiwa kwenye nafasi ya tisa kwa pointi nne, ikicheza mechi mbili tu.

Wakati huo huo, straika wa zamani wa timu hiyo, Dua Said na winga wa kushoto, Thomas Kipese ambao waliichezea timu hiyo miaka ya 1990, pamoja na mambo mengine, wamesema upangaji wa kikosi pia kwenye mechi hiyo ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Jwaneng Galaxy, haukuzingatia mahitaji ya mechi yenyewe.

"Nilikuwa uwanjani, mabao yote matatu iliyofungwa Simba yalikuwa rahisi sana. Ni mabao yanayofungwa kwenye mechi za kirafiki au bonanza, kwa sababu wachezaji hawajitumi sana, au kutoa jasho lao na kupambana. Nadhani makosa ni ya benchi la ufundi na wachezaji pia," alisema Dua.

Kwa upande wa Kipese yeye ametilia shaka viwango vya wachezaji wapya ambao wamesajiliwa.

"Walioondoka ni Luis Miquissone na Clatous Chama na wamesajili wachezaji wengi, inakuwaje pengo lishindwe kuzibika? Simba haikuwa na haja ya kusajili wachezaji wengi kiasi hiki. Wangesajili wachezaji wa viwango vya juu wawili tu kuziba pengo kwa sababu bado timu ni ile ile na nzuri," alisema.

## Mechi za usiku Dar ni bora - Mchezaji

**Na Adam Fungamwango**

HISTORIA iliandikwa Jumapili iliyopita, baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuchezwa usiku kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma huku nahodha wa Dodoma Jiji, Mbwana Kibacha, ambaye timu yake ilicheza dhidi ya Prisons, akibainisha tofauti kati ya kucheza usiku kwenye viwanja vya Dar es Salaam na viwanja vingine vya Tanzania Bara.

Kwenye mechi hiyo ambayo wenyeji walishinda mabao 2-1, kwa mara ya kwanza mechi ilichezwa usiku majira ya saa mbili, baada ya kukamilika shughuli za ufungaji taa.

"Kucheza usiku si jambo geni kwangu na hata wachezaji wenzangu, tumeshacheza mechi za usiku Dar es Salaam, tumecheza leo hapa, tumefurahi ni jambo jema, lakini kucheza usiku Dar unakutana na viwanja laini kwa hiyo mechi inakuwa nzuri sana na wachezaji mnafurahia mechi, huku viwanja bado vigumu na havipo kwenye hali nzuri, kwa hiyo hata kama mnacheza usiku, bado kunakuwa na ugumu fulani kutokana na matatizo ya viwanja. Kama vikitengenezwa na kuwa vizuri, basi hata wachezaji tufurahia," alisema nahodha huyo.

## Betika yafanya kweli Sodo Cup

**Na Saada Akida**

KAMPUNI ya kubashiri matokeo michezoni ya Betika, imetangaza kudhamini michezo ya soka mitaani maarufu 'chandimu', lengo likiwa ni kukuza vipaji vya wachezaji chipukizi kwa kuandaa mashindano ya yatakayojulikana kama 'Sodo Bingwa Awards'.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Masoko wa Betika, Flora Chacha, alisema katika udhamini wao, wamejipanga kutoa fedha na vifaa mbalimbali vya michezo ikiwamo jezi kwa timu zote zitakazoshiriki mashindano hayo.

Chacha alisema malengo makubwa ya kudhamini mashindano hayo ni kuwapa sapoti vijana wa mtaani ambao wanavipaji vya kucheza soka na wanahitaji kuendelezwa huku pia wakiinuliwa kiuchumi.

Alisema mashindano ya Sodo Bingwa kwa mwaka huu yamezinduliwa rasmi kwa soka la mtaani kwa kutumia soka la 'chandimu' pamoja na wachezaji kucheza bila viatu.

"Betika tunatambua mtaani kuna wachezaji vijana wengi wanapenda kucheza soka, hali hiyo imetusukuma tudhamini michuano hii kuhakikisha tunaendeleza vijana hao katika soka," alisema Chacha.

Alisema tayari mashindano hayo yamefanyika katika mikoa minne, ikiwamo Mbeya, Dodoma, Kagera na sasa yanafanyika Dar es Salaam na mipango yao ni kuendelea katika mikoa mingine.

"Baada ya kuzunguka katika mikoa hiyo, mwisho wa siku tutakuwa na mabingwa wa mikoa yote ili kupata bingwa wa nchi wa mashindano ya Sodo Bingwa Awards," alisema Flora.

**MAZOEZI...**




Wachezaji wa Timu ya Fedha FC, wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Hospitali ya Kivule jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Odhiambo atoa ya moyoni Biashara

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya Klabu ya Biashara United kushindwa kusafiriki kwenda kushiriki mchezo wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya timu ya Al Ahli Tripoli ya Libya, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Patrick Odhiambo, amesema kitendo hicho kimemwathiri kisaikolojia pamoja na wachezaji wake kutokana na maandalizi ya muda mrefu waliyoyafanya.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka mkoani Sumbawanga, walipo kwa ajili ya mchezo wao wa leo Ligi Kuu dhidi ya Tanzania Prison, Odhiambo alisema atakuwa na wakati mgumu kuwaweka sawa wachezaji wake kisaikolojia kuweza kurudia hali yao ya kawaida kama awali.

"Tangu tatizo hilo limetokea, sijazungumza na chombo chochote cha habari wala uongozi wangu kwa sababu nimeumia sana, tulijipanga kwa nguvu zote tukiwa na malengo ya kufika mbele katika mashindano ya kimataifa, lakini mipango yote imekufa," alisema Odhiambo.

Kocha huyo alisema malengo ambayo waliyapanga katika ushiriki wao wa mashindano ya kimataifa yangewabadilisha kwa kiasi kikubwa na kwamba michezo yote waliyocheza na kushinda ilikuwa migumu isipokuwa wachezaji walipambana mpaka kupata matokeo mazuri, kitu ambacho kimezidi kuwaumiza.

## ZISIKUPITE

### MO MSHAHARA MKUBWA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Misri, Mohamed Salah, 29, anataka mkataba atakaolipwa mshahara wa Pauni 500,000 kwa wiki, ili kusalia kwenye klabu hiyo. **(Football Insider)**

### SOLSKJAER KUTIMULIWA TRAFFORD

UONGOZI wa Manchester United unafikiria kumtimua Solskjaer kabla ya mechi ijayo ya Jumamosi ugenini, dhidi ya Tottenham Hotspur. **(Manchester Evening News)**

### ZIDANE HAITAKI MAN U

ZINEDINE Zidane hafikirii kuwania kazi katika Klabu ya Manchester United licha ya kutokua na timu tangu aondoke Real Madrid, Mei mwaka huu.

### UNITED HAICHEZI KITIMU

MANCHESTER United chini ya Ole Gunnar Solskjaer 'haichezi kitimu', amesema Micah Richards. Mnorway huyo amekalia kuti kavu kufuatia kipigo cha 5-0 kutoka kwa Liverpool. **(Football Insider)**

### GERRARD ATAJWA NEWCASTLE

MLINZI wa zamani wa Newcastle na timu ya vijana ya England chini ya miaka 21, Ryan Taylor mwenye umri wa miaka 37, amesema timu hiyo inapaswa kuzungumza na kocha wa Rangers, Steven Gerrard mwenye umri wa miaka 41, kuhusu kumpa mikoba ya kuwanoa matajiri hao wa St James' Park. **(Sky Sports)**

### CHALOBAH KUSAINI MKATABA

MLINZI wa Chelsea, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 22, anakaribia kusaini mkataba mpya wa muda mrefu baada ya kufanikiwa kuwa katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo. **(Football.London)**

### ZIDANE AITAKA PSG

ZINEDINE Zidane mwenye umri wa miaka 49, anaelekeza macho yake kukinoa kikosi cha Paris St-Germain au timu ya Taifa ya Ufaransa**. (Mundo Deportivo)**

### DE BEEK KUONDOKA UTD

KIUNGO wa Uholanzi, Donny van de Beek ameamua kubadili wakala wake akihaha kuondoka Manchester United katika majira ya baridi Januari huku Everton, Newcastle na Juventus zikionyesha nia ya kumtaka kiungo huyo mwenye miaka 24. **(Metro)**

### KOEMAN HATARINI BARCA

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman mwenye umri wa miaka 58, ataweka kibarua chake matatani kama kikosi hicho kitashindwa kupata ushindi katika michezo mitatu ijayo. **(Marca)**

### NAKAMBA AWANIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inamtaka kiungo wa Aston Villa na Zimbabwe, Marvelous Nakamba mwenye umri wa miaka 27, katika dirisha la Januari. **(Football Insider)**

### OLE APAMBANA UNITED

OLE Gunnar Solskjaer mwenye umri wa miaka 48, anapambana kuokoa kibarua chake kama kocha wa Manchester United na tayari raia huyo wa Norway ameshapoteza imani ya baadhi ya wachezaji hata kabla ya kipigo cha Jumapili cha mabao 5-0 kutoka kwa Liverpool. **(Manchester Evening News)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HENRY AFUNGUKA MAZITO YA MESSI KUTENGWA PSG

Siwezi kusema kwamba ana huzuni, lakini ametengwa, ningependa achezeshwe katikati, simwoni akiwa kwenye ubora wake...

**PARIS, Ufaransa**

LIONEL Messi "ametengwa" pale Paris Saint-Germain, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa zamani, Thierry Henry.

Messi aliwasili hapo kutoka Barcelona kama mchezaji huru mwanzoni mwa msimu huu, lakini mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or bado hajawa kwenye kiwango bora kwa miamba hao wa Ligue 1.

Huku Messi akiwa amefunga mabao matatu katika mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa na PSG, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, bado hajafunga wala kutoa asisti kwenye Ligue 1 msimu huu baada ya mchezo wa Jumapili wa 'Le Classique' dhidi ya Marseille.

Kwenye ligi, Messi ametengeneza nafasi kubwa moja ya kufunga huku akiwa na nafasi tano za wazi na Henry - ambaye alicheza na nyota huyo wa kimataifa wa Argentina pale Barcelona - ameelezea kinachomsibu.

"Yeye (Messi) ametengwa, hapewi nafasi kubwa," amesema nyota huyo wa zamani wa Arsenal na Ufaransa, Henry akiiambia RMC Sport.

"Siwezi kusema kwamba, ana huzuni, lakini ametengwa. Ningepeda yeye achezeshwe katikati.

"Huwa simuoni akiwa kwenye ubora wake, akicheza winga ya kulia. Akiwa katikati anaweza kufanya chochote atakacho.

"Wakati mwingine kuna mambo yanafanywa, ili kuwawezesha Mbappe, Neymar na Messi kucheza pamoja."

Henry ameongeza: "Nafikirii kama anaweza kutengeneza tofauti akiwa winga ya kulia, lakini sina taarifa kamili kutoka kwa kocha wake.

"Kwa kawaida akiwa katikati anaweza kuleta mchango mkubwa sana kwa timu. Lakini sasa anakuwa na mipira michache mno kwake."







# GIROUD ATAKA TAJI SERIE A NA MILAN



**MILAN, Italia**

MSHAMBULIAJI wa AC Milan, Olivier Giroud, malengo yake ni kushinda taji la Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa na Rossoneri hao.

Mshindi huyo wa Ligi ya mabingwa Ulaya msimu wa 2020-21, kabla ya kuondoka Chelsea kwenda Milan, Giroud hajashinda taji la Ligi Kuu tangu alipotwaa lile la Ufaransa, Ligue 1, akiwa na Montpellier msimu wa 2011-12.

Milan haijashinda taji la Ligi Kuu, Scudetto, tangu mwaka 2011 - kwa sasa wanaongoza msimamo wa Serie A pamoja na Napoli baada ya mechi tisa wakitoka kuwafumua 4-2 Bologna wiki iliyopita.

"Huwa napenda kusema soka ni mchezo, ambao unatakiwa mara zote kuwa tayari kwa changamoto mpya," alisema nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa Giroud, ambaye ana mabao matatu katika mechi tano za Serie A msimu huu akiiambia Football Ramble.

"Bado sijamaliza kazi kwa kushinda taji la Ulaya nikiwa na Ufaransa kule Ureno. Pia sikushinda taji la Ligi Kuu England nikiwa na Arsenal au Chelsea.

"Bado nina matumaini ya kushinda taji la Ligi Kuu na klabu yangu mpya, hayo ndio malengo yangu."

# Arteta asifia kiwango cha Aubameyang



**LONDON, Enfland**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anaamini Pierre-Emerick Aubameyang amerudi kwenye ubora wake kama mshambuliaji bora.

Baada ya kuanza vibaya msimu wa 2020-21, nahodha huyo wa 'Washikabunduki' hao, Aubameyang ndiye mfungaji bora wa klabu hiyo, kwenye Ligi Kuu akiwa na mabao manne katika mechi nane na kocha huyo amemsifia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, kwamba amerudi katika ubora wake.

Arteta anaamini straika huyo wa kimataifa wa Gabon, anajitoa kwa nguvu zake zote, kwa ajili ya kuisaidia klabu hiyo na amekuwa mchezaji aliyekamilika.

"Namuona sasa Auba amerudi kwenye ubora wake kwa kile anachokifanya sasa," alisema Arteta akiiambia tovuti ya Arsenal kabla ya mchezo wa jana Jumanne wa Kombe la EFL, dhidi ya Leeds United.

"Ukiacha mabao, kusherehekea akiwafunga, umeona namna anavyokimbia akiwa na mpira? Anaonyesha wazi kwamba yupo katika ubora na kiwango cha juu zaidi kwa sasa.

"Hiyo inaonyesha kwamba, ameshapita kwenye wakati mgumu na sasa amerudi katika ubora wake, ambao alikuwa nao mwanzo.

"Nina imani Auba msimu huu utakuwa bora zaidi kwake, kwa sababu sasa ni kama amekuwa mpya na anacheza vizuri zaidi akishirikiana na Alexandre Lacazette."

## HABARI MICHEZO


,207,580

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 30/10/21 | 17:00 | Watford vs Southampton | 3.11 | 3.41 | 2.27 |
| 02. 30/10/21 | 17:00 | Burnley vs Brentford | 2.80 | 3.20 | 2.60 |
| 03. 30/10/21 | 17:00 | Derby vs Blackburn | 2.57 | 3.16 | 2.71 |
| 04. 30/10/21 | 17:00 | Hull City vs Coventry | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 05. 30/10/21 | 18:00 | Metz vs St Etienne | 2.59 | 3.34 | 2.64 |
| 06. 30/10/21 | 19:30 | Tottenham vs Manchester Utd | 2.79 | 3.38 | 2.49 |
| 07. 30/10/21 | 19:30 | Valencia vs Villarreal | 2.86 | 3.36 | 2.45 |
| 08. 31/10/21 | 15:00 | Angers vs Nice | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 09. 31/10/21 | 16:00 | Cadiz CF vs Mallorca | 2.67 | 2.97 | 2.92 |
| 10. 31/10/21 | 17:00 | Bordeaux vs Reims | 2.43 | 3.19 | 2.94 |
| 11. 31/10/21 | 17:30 | Augsburg vs Stuttgart | 2.80 | 3.30 | 2.47 |
| 12. 31/10/21 | 19:30 | Aston Villa vs West Ham | 2.77 | 3.42 | 2.49 |
| 13. 31/10/21 | 22:45 | Roma vs AC Milan | 2.49 | 3.42 | 2.77 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 27 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2782 | Jubilo Iwata vs Oita Trinita | 2.09 | 3.15 | 3.34 |
| 13:00 | 3172 | Gangwon vs Daegu | 2.72 | 3.16 | 2.43 |
| 16:00 | 3921 | Bsk Bijelo Brdo vs Dinamo Zagreb | 20.32 | 8.13 | 1.08 |
| 16:00 | 4584 | Mlada Boleslav vs Viktoria Plzen | 3.14 | 3.33 | 2.10 |
| 16:00 | 4619 | Middelfart vs Randers | 8.15 | 5.24 | 1.28 |
| 17:00 | 5778 | Illichivec Mariupol vs Dynamo Kiev | 11.66 | 6.03 | 1.19 |
| 17:30 | 2763 | Banik Ostrava vs Hradec Kralove | 1.55 | 3.86 | 5.21 |
| 18:00 | 4819 | Teplice vs Sparta Prague | 7.16 | 4.84 | 1.34 |
| 19:00 | 1517 | Tromso vs Odd Ballklubb | 1.83 | 3.69 | 3.89 |
| 19:00 | 2603 | Mjondalen vs Kristiansund | 3.25 | 3.55 | 2.06 |
| 19:00 | 2696 | Sandefjord vs Stromsgodset | 2.15 | 3.60 | 3.01 |
| 19:00 | 3682 | Haugesund vs Rosenborg | 2.52 | 3.56 | 2.52 |
| 19:00 | 5824 | Lillestrom vs Stabaek | 1.53 | 4.44 | 5.13 |
| 19:30 | 1483 | Juventus vs Sassuolo | 1.51 | 4.52 | 5.85 |
| 19:30 | 2294 | Dynamo Dresden vs St. Pauli | 3.14 | 3.49 | 2.20 |
| 19:30 | 2379 | Bayer Leverkusen vs Karlsruher SC | 1.30 | 5.63 | 9.04 |
| 19:30 | 2654 | VfL Bochum vs Augsburg | 2.41 | 3.34 | 2.90 |
| 19:30 | 4381 | Sampdoria vs Atalanta | 4.12 | 4.12 | 1.76 |
| 19:30 | 5829 | Udinese vs Verona | 2.45 | 3.36 | 2.86 |
| 20:00 | 1931 | Mallorca vs Sevilla FC | 4.81 | 3.46 | 1.79 |
| 20:00 | 2092 | SKN St Polten vs RB Salzburg | 19.38 | 9.50 | 1.07 |
| 20:00 | 2288 | Slavia Prague vs Sigma Olomouc | 1.24 | 6.19 | 10.99 |
| 20:00 | 2773 | Ostersunds vs BK Hacken | 4.65 | 3.87 | 1.61 |
| 20:00 | 3398 | Malmo vs AIK Football | 1.69 | 3.58 | 4.45 |
| 20:00 | 3565 | Sirius FK vs Hammarby | 3.38 | 3.72 | 1.88 |
| 20:00 | 5958 | Rayo Vallecano vs Barcelona | 4.04 | 3.75 | 1.85 |
| 21:00 | 2930 | Molde vs Bodo Glimt | 1.98 | 3.83 | 3.24 |
| 21:00 | 5049 | Ismaily SC vs Al Ahly Cairo | 6.30 | 3.89 | 1.52 |
| 21:00 | 5785 | Betis vs Valencia | 1.86 | 3.62 | 4.13 |
| 21:00 | 5814 | Gvvv vs Sparta Rotterdam | 9.45 | 5.59 | 1.23 |
| 21:45 | 1002 | West Ham vs Manchester City | 5.75 | 4.26 | 1.50 |
| 21:45 | 1428 | Raal La Louviere vs Anderlecht | 17.62 | 8.61 | 1.10 |
| 21:45 | 1603 | Hibernian vs Celtic | 5.13 | 3.94 | 1.60 |
| 21:45 | 1703 | Monchengladbach vs Bayern Munchen | 6.62 | 5.22 | 1.39 |
| 21:45 | 2423 | Empoli vs Inter | 5.45 | 4.74 | 1.51 |
| 21:45 | 2515 | Burnley vs Tottenham | 3.12 | 3.37 | 2.19 |
| 21:45 | 2823 | Motherwell vs St Mirren | 2.43 | 3.14 | 2.89 |
| 21:45 | 2954 | Rangers vs Aberdeen | 1.31 | 5.10 | 8.84 |
| 21:45 | 3137 | Stuttgart vs FC Koln | 2.55 | 3.54 | 2.60 |
| 21:45 | 3345 | Dundee FC vs Ross County | 2.11 | 3.35 | 3.30 |
| 21:45 | 3771 | Hannover vs Fortuna Dusseldorf | 2.60 | 3.45 | 2.60 |
| 21:45 | 4026 | St Johnstone vs Hearts | 3.06 | 3.16 | 2.32 |
| 21:45 | 4445 | Cagliari vs Roma | 4.71 | 4.21 | 1.65 |
| 21:45 | 5386 | Leicester vs Brighton | 1.99 | 3.45 | 3.54 |
| 21:45 | 5587 | Preston vs Liverpool | 7.69 | 5.32 | 1.32 |
| 21:45 | 5730 | Stoke City vs Brentford | 2.91 | 3.31 | 2.33 |
| 21:45 | 5776 | Lazio vs Fiorentina | 1.94 | 3.71 | 3.71 |
| 21:45 | 5777 | Livingston vs Dundee Utd | 2.62 | 3.07 | 2.72 |
| 22:00 | 2638 | Nice vs Marseille | 2.43 | 3.33 | 2.83 |
| 22:30 | 4811 | Real Madrid vs Osasuna | 1.38 | 4.99 | 7.58 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# BARCA KUIVAA BOCA KOMBE LA MARADONA

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA watamenyana na Boca Juniors katika mchuano wa mkondo mmoja wa kirafiki, ili kuadhimisha mwaka mmoja tangu kufariki kwa aliyekuwa gwiji wa soka nchini Argentina na Klabu ya Napoli, Diego Maradona.

Vikosi hivyo viwili vitakutana Desemba 14, mwaka huu katika Uwanja wa Mrsool Park jijini Riyadh, nchini Saudi Arabia kwa ajili ya kivumbi hicho cha Kombe la Maradona.

Maradona aliwahi kuchezea Boca kwa awamu mbili na alistaafu akivaa jezi za kikosi hicho mnamo mwaka 1997.

Aliwahi pia kuvaa jezi za Barcelona kwa kipindi cha misimu miwili kabla ya kujiunga na Napoli mnamo mwaka 1984.


Maradona aliyeongoza Argentina kunyanyua Kombe la Dunia mwaka 1986, aliaga dunia Novemba 2020 akiwa na umri wa miaka 60, baada ya kupata matatizo ya moyo.

Akiwa Boca, Maradona aliongoza kikosi hicho kutwaa taji la Metropolitano mwaka 1981, kabla ya kushinda mataji akiwa na Barcelona ambako alitwaa Kombe la Mfalme (Copa del Rey), Copa de la Liga na Supercopa de Espana.

Alinyakuwa pia mataji mawili ya Ligi Kuu Italia (Serie A) akichezea Napoli na aliiongoza Argentina kunyanyua kombe la pili la dunia miaka 35 iliyopita nchini Mexico.

# Wanne watajwa kumrithi Solskjaer

**MANCHESTER, England**



KLABU ya Manchester United imewataja makocha wanne, ambao wanaweza kumrithi Ole Gunnar Solskjaer baada ya kipigo kikali cha mabao 5-0, kutoka kwa Liverpool kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Old Trafford, Jumapili.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Mail, matajiri wa Man United wanafikiria kuachana na kocha huyo wakati wowote kuanzia sasa.

Ripoti hiyo inasema kwamba, klabu hiyo ya Ligi Kuu England imemuagiza wakala mkuu kufanya mazungumzo na Antonio Conte, Zinedine Zidane, Brendan Rodgers na Erik ten Hag, iwapo Solskjaer atatimuliwa.

Wakala huyo ametakiwa kujua kila kocha miongoni mwa hao wanne kuwa na mipango, kwa ajili ya Man United na masharti yao ya mkataba.

Ripoti hiyo imesema kuwa mmoja kati ya makocha hao wane, ambaye atakidhi vigezo vya klabu hiyo atatangazwa kurithi mikoba ya Ole.

Wauaji wa Man United katika mchezo huo mwishoni mwa wiki walikuwa Mohamed Salah aliyefunga matatu dakika za 38, 45 na 50 huku mengine mawili yakifungwa na Naby Keita dakika tano na Diogo José Teixeira da Silva 'Diogo Jota' dakika 13.

# Michezo

Jumatano Oktoba 27, 2021

Nipashe





**Henry afunguka mazito ya Messi kutengwa PSG** UKURASA 21

KWAHERINI...




Aliyekuwa Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes (katikati) na wasaidizi wake, Kipa wa Makipa, Mbrazil Milton Nienov (kushoto) na Kocha wa Viungo, Mtunisia Adel Zrane. Makocha hao wameachishwa kazi rasmi jana. **PICHA: MAKTABA**

## Yanga sasa yaja na burudani kwa Mkapa

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga umesema katika michezo yao ya nyumbani sasa wataweka na burudani ya muziki ili kuwavutia mashabiki watakaoenda kushuhudia mechi zao, wakianza na dhidi ya Azam FC, utakaopigwa Jumamosi wiki hii kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Msemaji wa Yanga, Haji Manara, alisema wamekuja kivingine na kila mechi yao kutakuwa na burudani mbalimbali ikiwamo muziki wa kizazi kipya ili kuwapa burudani mashabiki katika michezo yote ya nyumbani.

Alisema kuelekea mchezo wao dhidi ya Azam FC wamejipanga vizuri na wana imani timu itakuwa na ushindani mkubwa kutokana na ubora wa vikosi vya timu zote mbili.

"Jumamosi tunaenda kukutana na wanaume wenzetu, tumewaona Azam FC wana wachezaji wazuri, tunatambua itakuwa mechi ya ushindani na tuna waheshimu, kikubwa tumejiandaa kwenda kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo," alisema Manara.

Alisema hawana majeruhi zaidi ya Dickson Ambundo, ambaye bado hajaanza mazoezi kwa sababu anaendelea kuuguza majeraha yake na wachezaji wengine wako vizuri na tayari kwa mchezo huo.

# GOMES AFUNGUKA MAZITO

## ●●●Ni wakati akitimuliwa na Simba ikipangiwa Wazambia CAF, nyuma ya pazia zamwagwa sababu kibao, huku...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba inashuka dimbani leo kuikabili Polisi Tanzania katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa klabu hiyo, umeachana na Kocha wao Mkuu, Didier Gomes, bila kutaja sababu, lakini Mfaransa huyo amefunguka mazito huku Nipashe ikipata za ndani kabisa tofauti na wengi kuaminishwa kuwa sababu pekee ni matokeo mabaya kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana.

Simba ambayo Jumapili iliyopita ilikubali kipigo cha mabao 3-1 dhidi ya Jwaneng Galaxy katika Uwanja wa Benjamin Mkapa licha ya mchezo wa awali ugenini kushinda 2-0, hivyo kufanya matokeo ya jumla kuwa 3-3 na kutolewa kwa faida ya bao la ugenini, imeangukia Kombe la Shirikisho Afrika na jana katika droo iliyochezwa Cairo, Misri, imepangwa kukutana na Red Arrows ya Zambia mechi ya kwanza ikipigwa Dar es Salaam Novemba 28 kabla ya kurudiana Desemba 5, mwaka huu.

Hata hivyo baada ya uongozi wa Simba jana kufikia maamuzi magumu kwa kumtimua Mfaransa huyo na wasaidizi wake wawili; Kocha wa Makipa, Mbrazil Milton Nienov na Kocha wa Viungo, Adel Zrane, Gomes alisema ameamua kuachia ngazi kwa sababu ya kuwajibika kutokana na matokeo mabovu ambayo timu hiyo iliyapata Jumapili.

"Nimeamua kuachia ngazi kutokana na kupoteza mechi dhidi ya timu ya Botwana (Jwaneng Galaxy) Jumapili, ilikuwa ni siku ya huzuni. Nimeamua kuchukua jukumu hili la kuwajibika kama kocha. Baada ya kuongoza bao moja tulipoteza nafasi nyingi za kufunga, tuliachia mianya na nafasi kubwa kwa wenzetu kucheza. Hatukukaba vizuri.

"Nawapongeza viongozi, wanachama na mashabiki wote wa Simba akiwamo Mwekezaji, Mohamed "Mo" Dewji, tulikuwa kwenye wakati mzuri, tulitwaa ubingwa na Kombe la FA, lakini Jumapili tukashindwa kuingia makundi. Nasema asanteni sana nawashukuru kwa sapoti yenu, nitaendelea kuwa shabiki wa Simba," alisema kocha huyo.

Lakini kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Simba jana jijini Dar es Salaam, inaeleza uongozi wa klabu hiyo umefikia hatua hiyo baada ya tathmini na majadiliano ya kina na pande zote zimeafikiana kwa mujibu wa mkataba na manufaa ya pande zote mbili.

Ilisema uongozi wa klabu hiyo, imekutana na Gomes kwa kujadiliana, kuridhia kuachana na kocha huyo, pamoja na kufanya mabadiliko madogo katika benchi la ufundi kwa kusitisha mikataba ya aliyekuwa kocha wa makipa, Nienov na kocha wa viungo, Zrane.

"Kutokana na hatua hiyo, aliyekuwa Kocha Msaidizi, Thierry Hitimana, ndiye atakuwa kocha mkuu wa Simba katika kipindi hiki cha mpito akisaidiwa na Seleman Matola. Simba inamshukuru Gomes na wenzake kwa mafanikio waliyopata katika kipindi walichoitumikia na kuwatakia heri katika majukumu yao mengine huko waendako," ilieleza taarifa hiyo.

Hata hivyo, taarifa nyuma ya pazi zilizolifikia gazeti hili muda mchache kabla ya kwenda mitamboni, zinaeleza kuachishwa kazi kwa Gomes kumetokana pia na kutengeneza makundi katika kikosi chake.

"Unajua kiufundi uongozi unamkubali sana Gomes, lakini umeona utumie mwanya huo kuchukua hatua mapema kutokana na kutowakubali baadhi ya wachezaji na kusababisha uwapo wa makundi kikosini.

"Gomes kuna wachezaji hawakubali kabisa licha ya kuonyesha uwezo mkubwa mazoezini, baadhi yao ni Ajibu [Ibrahim], Onyango [Joash], Mkude [Jonas], Kagere [Meddie] na Gadiel [Michael]," kilieleza chanzo chetu cha uhakika ndani ya Simba.

Kilidai Ajibu alionekana kama mbadala sahihi wa Clatous Chama na alipewa masharti mazito kuhakikisha anaongeza bidii mazoezini na kujituma zaidi kabla ya kusaini mkataba mpya, lakini licha ya kufanya hivyo Gomes amekuwa hamkubali.

Katika hatua nyingine, mbali na Simba jana kwenye droo ya Shirikisho la Soka barani Afrika iliyochezeshwa Cairo, Misri jana, na mabingwa hao wa Tanzania Bara, kupangwa na Red Arrows ya Zambia, timu nyingine za Ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati kwenye mechi hizo za mtoano kuwania kutinga hatua ya Makundi ya Kombe la Shirikisho ni TP Mazembe ya DR Congo, ambayo imepangiwa Marumo Gallants ya Afrika Kusini iliyowatoa ndugu zao, AS Vita, huku Gor Mahia ya Kenya ikipangwa na AS Otoho ya Angola, wakati DC Motema Pembe pia ya DR Congo imepangwa na USGN ya Nigeria. APR ya Rwanda yenyewe ikipangwa na RS Rerkane ya Morocco anayoichezea nyota wa zamani wa Simba, Clatous Chama.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >